
ICMinistries

Instruction in Bible Study ✝ Sermon Preparation

# Kuhusisha Wanaosoma Biblia

**Jinsi ya kusoma Biblia kupitia Maandiko kwa ufasaha**

## Kimetengenezwa
## kwa ajili
## Wachungaji na Wanaofanya kazi kanisani



Intensive Care Ministries • P.O. Box 109 • Mentone, CA 92359 • USA • (909) 798-0451 info@icmbible.org •www.icmbible.org

# KUHUSU KITABU HIKI CHA MWONGOZO

Kitabu hicho cha mwongozo kilitengenezwa na Mchungaji Dan Finfrock kwa muda wa miaka mingi akifanya kazi na maelfu ya wachungaji pamoja na watenda kazi Wakristo wengi katika nchi ya Ufilipino. Kimekusidiwa kuwasaidia viongozi jinsi watakavyojifunza Biblia, bila vitabu vya nje vingine, kama Maelezo ya Biblia na Biblia yenye Msaada kwa Watu n.k., ambavyo havipatikani katika maktaba za viongozi wa makanisa katika nchi zinazoendelea.

Kwa kutumia Maandiko Matakatifu yaliyotafsiri vizuri, kila mshiriki atafundishwa jinsi atakavyochungaza, fafanua na tekeleza Neno la Mungu kwa uangalifu. Maandiko yatakuwa halisi kupitia mfumo huu unaosisimua na ulioitwa Kuhusisha Wanaosoma Biblia. Mfumo huo ni mafunzo yanayofaa kujifunza Maandiko Matakatifu kwa ukamilifu, tena yenye utaratibu.

Kitabu hicho cha mwongozo kimetumika kumfundisha ye yote anayetaka kujifunza jinsi atakavyosoma Neno la Mungu kwa kufaa. Kinatumika katika nchi nyingi na kimetafsirika katika lugha zaidi ya ishirini ulimwenguni.

# KUHUSU MWANDISHI

Mchungaji Dan Finfrock alilelewa katika Kanisa la Ushirikiano wa Wamisionari Wakristo kule mji wa Redlands, mkoa wa California, USA. Baadaye akasoma katika Chuo cha Biblia Simpson cha Ushirikiano huo. Baada ya kuhitimu Chuo Kikuu cha Redlands, akaanza ku-fanya kazi katika Inter Varsity Christian Fellowship (yaani Ushirikiano Wakristo katika Vyuo Vingi) kwa muda wa miaka sita akifundisha 'Kuhusisha Wanaosoma Biblia' katika maeneo ya vyuo. Halafu akaingia kazi ya uchungaji akihudumia katika makanisa sita, tatu ya hayo yalikuwa makanisa yaliyoanzishwa nao. Kanisa lake la mwisho liliitwa Calvary Chapel (yaani Kanisa la Kalvari) kule Banning.

Mwaka 1985 Mch Dan alihamia Ufililpino, pamoja na familia yake, akaanzisha Intensive Care Ministries [ICM kwa kifupi] (yaani Huduma ya Uangalizi). Akaona kwamba wachungaji wenyeji wanahitaji mafunzo jinsi watakavyosoma Neno. Mfumo wa Kuhusisha Wanaosoma Biblia umefanya kazi vizuri, tena umefunzwa kwa haraka. Mwaka 1991, familia yake yote wakarudi USA, na wakati ule akaanza kazi ya kusambaza mfumo huo katika nchi nyingi nyingine. Urusi ilikuwa eneo muhimu muda wa miaka minane iliyopita. Sasa ICM ina watenda kazi sita Warusi wanaofanya kazi katika sehemu mbalimbali. Mch Dan anaishi mji wa Mentone, California pamoja na mke wake, aitwaye Debbie, na mtoto wa mwisho, anaitwa Aaron. Wana watoto watatu ambao wameshakua pengine, wanaitwa Nathan, Lela na Corrie. Mch Dan anasafiri nchi nyingi zinazoendelea.

Imeandikwa tarehe 20 mwezi wa 9, mwaka 1999

# INTENSIVE CARE MINISTRIES

## TAARIFA YA IMANI YETU

1. Tunaamini ya kuwa upendo wa Mungu ni kwa kila mtu na kwa ajili ya upendo wake, alimtuma Yesu aje duniani na afe msalabani kwa ajili ya dhambi za wanadamu, na ya kuwa alifufuka siku ya tatu.

   KWA HIVYO: Tunatangaza msamaha wa dhambi na Bwana aliyefufuka.

2. Tunaamini ya kuwa maandiko yote yanatokana na Roho ya Mungu huku yakifaa kwa mafundisho, kuwaonya watu makosa yao, kuwaongoza, kuadhibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, apate kutenda kila tendo jema. 2 TIMOTHEO 3:16 na 17.

   KWA HIVYO: Tunasisitiza mafundisho ya Neno.

3. Tunaamini ya kwamba Mungu amewainua watu na kuwapa vipawa kwa ajili ya utayari-shaji wa mwili wa Kristo upate kukua na kufikia ukomavu wa Kristo. WAEFESO 4: 11-16

   KWA HIVYO: Tunawatafuta watu walio na vipawa tukiwaandaa kufundisha Neno.

4. Tunaamini katika kurudi upesi kwa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo

   KWA HIVYO: Tunaenenda na kufanya wanafunzi kwa watu wa mataifa yote MATHAYO 28:19

5. Tunaamini ya kwamba mwili wa Kristo ni mmoja ijapokuwa kanisa lake lina matawi, na kwa kazi ya Roho mtakatifu sote tu umoja katika Kristo.

   KWA HIVYO: Tunatunza kwa bidii ule umoja wa Roho. WAEFESO 4:3

## TAARIFA YA MAONO YETU

Misingi ya huduma hii ya Intensive Care Ministries, imewekwa katika kutayarisha wachungaji na watenda kazi wa Kristo kwa ajili ya kazi ya utumishi. Malengo yetu ni mawili: 1) Kuwafundisha jinsi ya kujifundisha Neno na 2) Kuwahimiza walishe watu wao kwa kujifunza Biblia kwa mpangilio. Maono yetu ni kuzindua ukufunzi katika nchi kadha wa kadha mpaka tutimize makusudi haya.

Yaliyomo


**Kuhusu Semina ……………………………………………………………5**

**Vitabu vya Biblia ……………………………………………………..6**

**Njia za kujifunza Biblia ………………………………………………7**

Maelezo juu ya

Uchungaji ……………………………………………………………………..8

Ufafanuaji ……………………………………………………………………..9

Utekelezaji ……………………………………………………………………..12

**Chanzo cha kufundishia Biblia…………………………………...13**

Mazoezi:

1. Usimulizi ………………………………………………………………………..16
2. Ushairi ………………………………………………………………………….19

   Kujifundisha Biblia kwa Kuzoesha ………………………………......20

3. Nyaraka ……………………………………………………………………....25
4. Mashairi ya Waebrania ………………………………..………………..28
5. Maswali ya mazoezi ……………………………………………….……32
6. Mifano ya Yesu ……………………………………………..…………..…36
7. Unabii ……………………………………………………………………..……40

Kazi ya Mazoezi:


8. Usimulizi/Yohanna 13……………………………………………..…46
9. Nyaraka-Filemoni……………………………………………………….49
10. Unabii-Isaya 55…………………………………………………………….50

Kiambatanisho:

11.Jinsi kuanzisha na kuongoza mafunzo ya Biblia………………………52-61

12.Mfano wa wahubiri ya ufafanuzi kwa kujielezea……………………...62-66

# Muhtasari Kuhusu Washa



Muundo wa kimaandiko wa Biblia:

1. Usimulizi
2. Nyaraka
3. Mifano
4. Ushairi
5. Unabii


## Maudhudhi ya Vifungu

1. xxxx xxx xx xxx
   a. xx xxxx xx
   b. xxx xx xxxx
2. xx xxxxx xxx xx x

| Uchunguzi | Ufafanuzi | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 1. xxx xx xxxxx | Xxxxxx xxx xx xxxx | Xx xxxx xxxxxx xx xxx xxxx x xxxx xx x xxxx x xxx x xxx xx x xxxxxx x xx |
| a. xx xxxx<br>b. xxxx xxx<br>c. xx xxxxxx<br>d. xx xxx | Xxxxxxx xx xx xx xxx xxxx xxx x xxx xxxx xx xxxx | |
| 2. xxx xxxxxx | | Xx xxxx xxxxx x |

**Mahubiri - Maudhudhi**

1. xxxx xxx xx xxx
   c. xx xxxx xx
   d. xxx xx xxxx
2. xx xxxxx xxx xx x




**Hotuba**

**Maswali ya unchunguzi**

1. xxxx xxx xx xxx
   a. xx xxxx xx
   b. xxx xx xxxx
2. xx xxxxx xxx xx x




**Mafunzo ya Biblia**




# VITABU VYA BIBLIA

**Funza Biblia nzima. Kumbuke ujumbe wa mwisho wa Paulo kwa wazee wa Efeso, "Kwa kuwa sikuwaficha kuwaambiani *ushauri wote wa Mungu*." Mdo 20:27**




# Mbinu za Kujifundisha Biblia

**Njia tatu zinazotumika zaidi katika kujifundisha Biblia ni:**

- **Utafiti** – "Kuonyesha mambo ya asili"
- **Utafutaji** – "Kuanza kwa dhana iliyoko"
- **Mada Inayohusiana** – "Kushirikiana maoni yaliyoko"

***KUMBUKA! "Fuatilia Utaritibu"------- "Fuatilia Wazo"***





# Maana ya

| Uchunguzji | Ufafanuzi | Utekelezaji |
|---|---|---|

***Je, Kifungu kinasema nini?***

- Soma kifungu zaidi ya mara moja
- Nakili fikira za kwanza unazopata
- Andika(nakili)ya kuwa inahusu Nani, Nini, Lini na Wapi




# Maana ya

| Uchunguzaji | **Ufafanuzi** | Utekelezaji |
|---|---|---|

***Je, Kifungu kina maana gani?***

- Chambua kifungu kinenavyo
- Jifunzie katikati ya maneno yaliyomo katika kifungu
- Andiko lifafanue andiko lingine
- Agano jipya lipewe utangulizi

# Maelekezo zaidi ya ufafanuzi.

Ni lazima tufuate maelekezo fulani tukitaka kufahamu Neno la Mungu sawa sawa. Ingawa kufuata maelekezo mengine haitatuhakikishia uamuzi barabara, kuyapuuza husababisha upotovu.

## Yafuatayo ni baadhi ya masharti ya kwanza;

**I. FAFANUA UJUZI WAKO KIMAISHA KWA MAANDIKO: USIFAFANUE MAANDIKO KWA UJUZI WAKO.**

Watu wanapotumia ujuzi wao wa kimaisha kufafanua maandiko ndio ujuzi kwa mamlaka kamili kwao. Neno la Mungu ni kamilifu na maisha yetu yamo mamlakani mwa maandiko.

Mkristo anapotaka wengine kwa jumla waenende katika njia iliyomfaa yeye binafsi, ndipo anapoingia katika hatari ya kukaidi kanuni, licha ya kuwa ni tekelezo la amri ya Biblia. Mfano mzuri ni mtu yule aliyekataa tabia ya kununua chochote kwa njia za mkopo. Mtu huyu alifaulu sana kuacha tabia hiyo lakini alianza kuwalaumu waliokuwa na hati za deni na kununua kati ya muda uliotolewa akisema hivyo ni kukaidi agizo la Biblia (Rum 13:8). Hali hii ni ya mtu mmoja anayefafanua maandiko kwa ujuzi wake, huku akihalalisha ujuzi kuwa kamili badala ya maandiko.

**II. USIANDAMANE NA SHAURI UKAACHANA NA MAANDIKO.**

Katika sura zake nyingi Biblia haikati shauri. Jihadhari kuena zaidi ya Biblia inenavyo. Katika mambo ya binafsi, hasa mitindo ya mavazi, viwango vya maisha au maongozi kanisani ni lazima mtu akate shauri ingawa maandiko hayaneni hayo. Tunaweza kufuata maoni yetu lakini tusiwaonee wenye maoni mbali na yetu. Tunahitaji kuwapenda wenye maoni mbalimbali.

**III. ELEWA KAMA KIFUNGU NI FANANISHO AU NI HALISI.**

Imetupasa kuchukua kifungu kuwa mfano Biblia inaponena hivyo. Mara nyingi Biblia huonyesha ya kwamba kifungu ni fananisho au halisi pia. Wagalatia 4 inanena mlima Sinai kuwa alama ya ufungwa, na Yerusalemu ni alama ya neema. Kijographia panaponenwa ni halisi na ni fananisho za ukweli wa kiroho pia. Tena kifungu ni fananisho ikiwa maneno yaliyomo ni ya sifa za kando na zile za kitu kinacho nenewa. Kwa mfano kifungu fananisho panapolinganishwa kitu kisicho hai na mtu au kingine chenye uhai katika Injili ya Yohana, inaonyesha Yesu ameonakana kuwa ni 'mlango', 'mkate', 'maji', n.k. haya yote ni maneno ya unafanishi. Wafilipi 3:2 Paulo anaonya "Jihadharini na mbwa", yaani wale wapotoshi wanaofundisha kwamba ni lazima kutahiriwa katika wokovu. "Mbwa" ni fananisho. Yesu anasema hakika (Luka 13:32) "nendeni mkamwambie yule mbweha." yaani Herode. Huu ni ufananishi.

Mara nyingine eneo lililotumika kwa mfano, linaweza kuwa na maana mbalimbali katika Biblia. Kwa mfano 'simba' katika 1 Pet 5:8 inasema Shetani; bali katika Ufunuo 5:5 inanena juu ya Yesu Kristo. Kama kawaida maana ya mfano itapatikana katika kifungu kamili.

Neno moja haliwezi kuwa halisi na fananisho kwa wakati mmoja. Neno la mstari linaposemwa kuwa fafanisho huwa limezidi maana yake halisi. Ikiwa ufafanuzi halisi unafaa basi lifafanuliwe hivyo, isipokuwa kifungu kikionyesha kwamba haiwezekani.

## IV. USIFAFANUE MAANDIKO KWA MAWAZO YA ELIMU YA KISASA.


Tusijaribu kufafanua maandiko kwa kutumia falsafa na maswala ya utafiti wa kisasa. Mawazo hayo hubadilika muda unaoendelea. Biblia hata hivyo, haibadiliki milele. Kwa miaka mingi wanahistoria wamekejeli Biblia kwa sababu haukupatikana ushahidi wa utafiti (archaeology) wa taifa la Wahiti linalotajwa. Katika Biblia lilikuwepo. Hapo katika mwaka 1907, watafiti waligundua ushahidi, yaani matofali fulani, huko Uturuki, yaliyo thibitisha kuwepo kwa taifa la Wahiti.

Haipasi sisi kuomba radhi kwa ajili ya maneno ya Biblia yasiyodhibitishwa kisayansi au kufafanua maandiko tena ili kuyaatia maana inayodhibitishwa na utafiti wa kisasa. Kwa sababu Biblia ni Neno la Mungu na ni kweli halisi; kila muujiza na kila neno yapaswa kusadikika.

**V.** Wanapojaribu kuupata "ukweli wa kiroho" katika kila mstari, wengi huingiza shauri la kweli ndani ya kifungu, ambalo limepatikana kwa njia isiyo sahihi. Mtu anapotumia njia isiyofaa kufikia uamuzi wa kweli, ataweza kujidanganya kwamba ataitumia isivyofaa.

Kwa mfano, Matendo ya Mitume mlg 28 imesema jinsi Paulo alivyopona kwa muujiza baada ya kuumwa na nyoka yenye sumu. Anayetafuta maana ya kiroho anaweza kusoma, hivi au yule nyoka ndiye Shetani anayeshambulia watauwa, lakini kila anapojaribu hushindwa.

Ushauri huu huenda ikawa ni kweli na ni fundisho kutoka kifungu kingine cha maandiko, bali Matendo 28 haifundishi hivyo. Hii ni njia potovu ya kushughulikia Neno la Mungu.




# Maana ya

| | | |
|---|---|---|
| **Uchunguzaji** | **Ufafanuzi** | **Utekelezaji** |

## *Ni jinsi gani nitakavyoitika?*

- Je, kuna mifano gani nitakayo ifuata?
- Je, kuna dhambi nitakayoacha?
- Je, ni makosa gani nitakayoepuka?
- Je, ni ahadi gani nitakazoamini?
- Je, ni amri gani nitakazotii?
- Je, ni matendo gani nitakayoyatenda?

## CHANZO CHA KUJIFUNZA BINAFSI

| ***Miundo*** | ***Miundo Usimulizi*** | ***Miundo ya Maagizo na maonyo (nyaraka)*** | ***Miundo ya Mashairi, Mifano, Ufunuo wa kinabii.*** |
|---|---|---|---|
| **MFANO** | Historia – nakala ya matukio kama vile Injili Matendo, Kutoka, Walawi, Hesabu, n.k. na Wafalme. | Ukuuzaji wa fundisho kwa welekevu – Nyaraka za Paulo: Wagalatia, Warumi, Tito n.k.<br>Maandiko ya Petro Yohana, Yakobo, na baadhi ya nakala za mafundisho ya Yesu. | Mpango wa mawazo kwa mbindo. Walitumia mifano na fani kufikisha wazo. k.v. Zaburi, Wimbo ulio Bora Isaya, Yeremia, na mifano ya Yesu n.k. |
| Sifa kuu za miundo | Watu, mahali, matukio na hisia | Mawazo, maneno, viarifa mafunzo, malengo na mipango ya vifungu | Angalia alama inayowakilisha jambo, fananisha, au inayolinganisha.<br><br>Lugha ya picha |
| ***Vifaa vya Msingi:***<br><br>***kwa***<br>**UCHUNGUZI** | Uliza<br>➢ Nani?<br>➢ Nini?<br>➢ Lini?<br>➢ Wapi?<br>➢ Vipi?<br><br>Eleza tena (tukio) hadithi<br><br>Tafuta uhusiano kati ya wahusika.<br><br>Jaribu kushika hisia zao.<br><br>Jiweke katika nafasi ya wahusika.<br><br>*Unaona nini? unahisia nini? unafikiri nini?* | Faharisi ukuuzaji wa mawazo katika kifungu.<br>Angalia mawazo yaliyorudiwa.<br>Tafuta:<br>Vilinganishi<br>Vibainishi<br>Maunganishi k.v.<br>➢ Kwa hivyo (ndiposa)<br>➢ Ili kwamba<br>➢ Kwa sababu<br>➢ Kwa ajili<br>➢ Hapo<br><br>Kila neno ni muhimu katika kufahamu kifungu kizima | Washairi wa kiebrania walitumia mdufya yaani wazo moja likiwasilishwa kwa njia mbili tofauti.<br><br>Methali ni msemo ambamo tabia ya mwana damu imelinganishwa na kiumbe cha asili. k.v.. Methali 5:3<br><br>Mfano ni muundo wa fasihi aliyotumia Yesu kuficha ukweli kwa watu wasiotaka kusikia neno.<br><br>Ufunuo wa unabii husemea mafunuo yatokayo kwa Mungu kuhusu matukio yajayo au yaliyopo sasa. |

## **CHANZO CHA KUJIFUNZA BINAFSI** (kuendelea)

| | |
|---|---|
| ***Vifaa vya msingi:***<br><br>*kwa*<br><br>**U<br>F<br>A<br>F<br>A<br>N<br>U<br>Z<br>I** | **<u>Vifaa vya ufafanuzi ni vile vile katika miundo yote mitatu.</u>**<br><br>Ni jaribio la kufafanua maana ya kifungu kwa wasikiaji wa kwanza.<br><br>1. Mwandishi anamaanisha nini kuandika alivyofanya?<br>➢ Ona<br>➢ Hisi<br>➢ Fikiri<br>2. Kwa nini anayaandika haya?<br>3. Ilikuwa na maana gani katika wakati na desturi zao?<br>Baadhi ya vifaa ni bora vinapotuumika kwa miundo wa maagizo na maonyo.<br>a Kwa nini wazo hili linatumika?<br>b Kwa nini mwandishi amelitumia?<br>c Je, angeweza kutumia neno lingine?<br>d Je lina maana gani?<br>e Ni uhusiano gani ulioko kati ya hili wazo na yale yalitotangulia?<br>f Sura nzima ni ya muhimu kuliko yote. |
| ***Vifaa vya msingi:***<br><br>*kwa*<br><br>**U<br>T<br>E<br>K<br>E<br>L<br>E<br>Z<br>A<br>J<br>I** | **<u>Vifaa vya utekelezaji ni vile vile katika miundo yote mitatu</u>**<br>1. Mwombe Roho Mtakatifu mafundisho 1Kor 2:9-16<br>2. Tekeleza dondoo muhimu maishani mwako k.v.<br>Je, kuna mfano ninaoweza/tunaoweza kuiacha?<br>Je, kuna dhambi ninahitaji/tunahitaji kuiacha?<br>Je, kuna makosa ninapaswa/tunayopaswa kuepuka?<br>Je, kuna ahadi ninayopaswa/tunayopaswa kuiamini?<br>Je, kuna amri ninapaswa/tunapaswa kuitii?<br>3. Sasa nini?<br>Ninapanga kufanya nini kuhusu haya?<br>Ni tofauti gani haya yataleta maishani mwangu?<br>Ni mipango gani hasa ninayoweza kufanya maishani?<br>Nitafanya nini?<br>Nitafanya jinsi gani? |

# MAZOEZI

# Vifungu Vya Usimulizi

Viko vitabu vingi katika maandiko vilivyoandikwa kwa muundo wa usimulizi. Hadithi hizi zinaeleweka kwa urahisi. Katika Agano la Kale hadithi inajumlisha Torati (Mwanzo – hadi Kumbukumbu la Torati) na vitabu vya historia, kama Yoshua hadi Esta. Vinajumlisha kutoka katika Agano Jipya, Injili zote na Matendo.

Kwa haya mazoezi ya kwanza, utahijika kujibu maswali yenye uhusiano na kifungu. Maswali hayo yametengenezwa kuonyesha mfano wa maswali ya kushawishi. Katika mazoezi yatafuata haya, yakuwa ya kuunda maswali ya kushawishi.

## ZOEZI :1

1. Soma kifungu (Marko 2:1-12) zaidi ya mara moja. Chukua muda kukichunguza kwa makini.

2. Jibu maswali yaliyo katika ukurasa unaofuatia. Hakikisha umemaliza zoezi. Usipoteze muda mwingi kwenye swali moja.

# MARKO 2:1 – 12 (Kifungu)

1. Akaingia Karpenaumu tena, baada ya siku kadha wa kadha, ikasikiwa ya kwamba yumo nyumbani.
2. Wakakusanyika watu wengi, isibaki nafasi hata mlangoni, akawa akisema nao neno lake.
3. Wakaja watu wakimletea mtu mwenye kupooza, anachukuliwa na watu wanne.
4. Na walipokuwa hawawezi kumkaribia kwa sababu ya makutano, waliitoboa dari pale alipokuwapo na wakiisha kuivunja wakalitelemsha godoro alilolilalia yule mwenye kupooza.
5. Naye Yesu alipoiona imani yao, akamwambia yule mwenye kupooza, Mwanangu, umesamehewa dhambi zako.
6. Na baadhi ya waanndishi waliokuwako huko, wameketi, wakifikiri mioyoni mwao.
7. Mbona huyu anasema hivi? Anakufuru. Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja ndiye Mungu?
8. Mara Yesu akafahamu rohoni mwake kwamba wanafikiri hivyo nafsini mwao akawaambia, Mbona mnafikiri hivi mioyoni mwenu?
9. Vyepesi ni vipi, kumwambia mwenye kupooza, Umesamehewa dhambi zako au kusema Ondoka ujitwike godoro lako, uende?
10. Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi (hapo akamwambia yule mwenye kupooza)
11. Nakuambia, Ondoka, ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako.
12. Mara akaondoka, akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote hata wakastaajabu wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, Namna hii hatujapata kuona kamwe.

# Maswali yanayohusu Marko 2:1-12

Uch. 1. Ni watu ganii waliotajwa katika hadithi hii?

Uch. 2. Katika hii je, Yesu alikuwa wapi wakati huo?

Uch. 3. Ni nini kilichotendeka? Eleza hadithi yote kwa maneno yako.

Ufa. 4. Ni nini baadhi ya shida za kimwili za mtu aliyepooza?

Uch. 5. Ni ugumu gani angepata akitaka kufika kwa Yesu?

Ufa. 6 a.) Hawa watu wanne walikuwa wa namna gani?

Ufa. 6 b) Kwa nini hakukata tamaa?

Ufa. 6 c) Yesu alisema juu ya imani ya nini wakati huu?

Ufa. 7. Kwa nini Yesu alisema “mwanangu dhambi zako zimesamehewa?”

Ufa. 8. Waandishi wanauliza nini kuhusu maneno haya ya Yesu?

Ufa. 9. Yesu alianza kijibu maswali yao wakati gani?

Ufa. 10. Soma mstari 9-11 tena. Ni lipi rahisi kusema? Kwa nini?

Ufa. 11. Ni mambo gani yaliyoko tunapolinganisha dhambi na kupooza?

Ufa. 12. Mtu aliyepooza ni kama nini hasa?

Ufa. 13. Kristo huwatendea nini wenye dhambi?

Ute. 14.a) Je unayo imani ya kembeba mtu aliyepooza kwa kristo.

Ute. 14.b) Orodhesha njia mwafaka za kufanya hivyo.

Ute. 15. Orodhesha baadhi ya njia za kuponyesha nakuwajali wenye dhambi.

Ute 16. Unawezaje kufaya kazi pamoja na wengine kuleta watu kwa Yesu.

**WEWE NI MJUMBE KWA WATU. KUMBUKA KWAMBA DHAMBI HUPOOZA.**

# Ushairi

Mashairi ya Kiebrania yamejazwa lugha ya mifano (isiyo halisi). Lugha hii huwasilisha mawazo kupitia matamshi ya maneno na semi zinazoumba picha kwa msomaji.

Alama ya kutofautisha ushairi wa Kiebrania na mengine ni ule uambatanishaji wa mfanano wa mstari kwa ule ufuatao au sura kwa ile ifuatayo. Marudio ya mawazo (maoni) kwa kurudia rudia husaidia kulea aliyomaanisha mwandishi. Tutachunguza baadhi uambatanishaji wa aina mbali mbali katika mazoezi ya baadaye.

Katika mazoezi haya, utaweza kujifunza ushairi rahisi. Kwanza unapaswa kujua vifaa viwili muhimu utakavyotumia katika kujifunza Biblia (IBS). Vifaa hivi ni kuorodhesha maudhui kufaharisi na kuunda vyanzo.

# KUJIFUNZA BIBLIA KWA NJIA YA UTAFITI

## KUCHANGANUA KIFUNGU CHA BIBLIA

Wazo kuu.

Kuchanganua waraka.

Kuchanganua Miundo mingine.

## MPANGANGILIO WA KIFUNGU

Cha Biblia kwenye Jedwali

Wazo kuu

Mfano wa kupangalia kifungu cha Biblia kwenye Jedwali

---

1. **KUCHANGANUA**: Kusudi la kuchanganua ni kuchunguza kifungu kwa makini. Kuna njia mbali mbali ya kuchanganua kusudi lake hasa ni kugawanya yale mawazo yaliyo-tolewa. Ni lazima kila wazo litengwe ili lifahamike barabara. Hapa tunajifunza njia mbili (2) za kuchanganua.

   A. Njia “rahisi” ya kuchanganua inayoweza kutumika kwa kitabu chochote cha Biblia.

   B. Kuchanganua “Nyaraka” inayorahisisha kazi ya nyaraka.

A. **MPANGILIO RAHISI**. Muundo huu ni rahisi kutumika kwa kurahisisha kitabu chochote cha Biblia. Unapitia kifungu cha Biblia kwa nia ya na kutafuta wazo/ mawazo yanayoongelewa.

Kwanza, kuangalia wazo, linapoanzia na kuamalizikia kifungu. Zifuatazo ni hatua za kimsingi za faharisi chunganuo.

| | |
|---|---|
| HATUA 1 | Andika kwa ufupi juu ya kiini cha kifungu. |
| HATUA 2 | Orodhesha dondoo ya kifungu ukiambatanisha mistari yake katika kifungu. |

**Kila unapochanganua fuata utaratibu wa mstari kwa mstari.**

# (MIFANO YA MCHANGANUO RAHISI)

## ZABURI 128

KIINI: Kumcha Bwana ni vema.

I. Matokeo ya kumcha Bwana Mst. 1 – 4

II. Matokeo ya furaha Mst. 5 – 6

## EZRA

KIINI: Marejeo Ya Ujenzi wa Hekalu

I. Marejeo ya ujenzi chini ya usimamizi wa Zerubabeli Sura 1 – 6

*A. Mateka wa kwanza warejea Sura 1 – 2*

*B. Marejeo ya ujenzi wa Hekalu Sura 3 – 6*

II. Mageuzi chini ya uongozi wa Ezra Sura 7 – 10

*A. Mateka wa pili warejea Sura 7:1 –8:32*

*B. Maguzi " Marejeo ya ujenzi wa watu (taifa)" Sura 8:33 – 10:44*

B. **UCHANGANUZI WA NYARAKA.** Nyaraka nyingi zimeandikwa zikifuata utaratibu wa mawazo, kama iandikwavyo barua (isipokua Waebrania na 1 Yohana). Unaposoma nyaraka angalia **utangulizi** wa barua hiyo – salamu zilizo hapo mwanzo (pengine hufuatwa na sehemu ya shukrani). Haya hufuatwa na **kusudi** la kuandika, **mafundisho** makuu na **kumalizia**.

1. **Utangulizi**. Mistari ya kwanza michache ya kifungu ni utangulizi na salaamu. Haya pengine hufuatwa na sehemu ya shukrani.

2. **Kusudi la Kuandika**. (Kwa nini barua inaandikwa?) Mara nyingi kusudi la kuandika barua huelezwa mistari miwili au mitatu. Kwa kawaida ni fupi na hufuata utangulizi (yaani salamu na shukrani) . Tafuta kwa uangalifu habari hii kwa sababu ndicho kifunguo cha barua.

3. **Fundisho maalum**. Moyo wa waraka unapatikana hapa. Utapata kwamba mawazo mbalimbali au masomo yatakuzwa kwa vifungu vinavyofuata. Pengine wazo huwekwa katika mistari michache au sura moja au zaidi. Kumbuka – si lazima sura au mgao wa mistari katika Biblia zetu ziwe mgao sahihi wa mawazo. Tafuta mawazo kwa mfano katika waraka mmoja mst. 5-10 inanena juu ya upendo, mst. 11-16, juu ya hukumu au furaha n.k.

4. **Kufunga (kumaliza).** Kila mara kifungu humaliza mawazo yakufunga pengine tunayatumia makanisani mwetu kama salamu za kuagana.

# (MFANO WA UCHANGANUZI WA WARAKA)

## TITO

| | | |
|---|---|---|
| I. UTANGULIZI | Sura 1:1-4 | Paulo akimwandikia Tito |
| A. Sura 1:1-4 | *Salamu* | |
| B. (*Hakuna*) | *Shukrani* | |
| II. KUSUDI LA KUANDIKA (Sababu ya Kuandika) | Sura 1:5 | Mawili – Kutekeleza mpango wa hudumu makanisani na kuwachagua viongozi wazee |
| III. FUNZO KUU | Sura 1:6-3:14 | Kuwachagua wazee na kuweka mwongozo kanisani |

*Mawazo matatu makuu:*

i. *Sura 1:6-16* — *Wazee. Hatima na kazi zao.*
ii. *Sura 2:1,3:11* — *Wajibu wa Kikristo kanisani na Mafundisho*
iii. *Sura 3:12 – 14* — *Mambo ya kibinafsi*

IV KUFUNGA — Sura 3:15

II. **KUTENGENEZA JEDWALI.** Ukiisha changanua kifungu, uko tayari kukigawanya zaidi kwa kuchanja. Mchanganuo hutumika kuangalia kifungu kwa mtambo wa UCHUNGUZAJI, UFAFANUZI, na UTEKELEZAJI (IBS). Chukua kila sehemu ya changanuzi mstari kwa mstari ukinakili maneno, misemo na mawazo katika kifungu kizima.

**(Yafuatayo ni mfano wa jinsi inavyotayarishwa)**

# WAFILIPI 1:1 – 6

| **UCHUNGUZAJI (UCH)**<br>(**Sema maneno** yaliyomo kwenye kifunguni maneno na mawazo muhimu) | **UFAFANUZI (UFA)**<br>(**Eleza** maana hapa) | **UTEKELEZAJI (UTE)**<br>(**Tekeleza** kwa jumla na kwa umoja) |
|---|---|---|
| **1.) Wazo mst 1-2 mistari**<br>*Hii ni utangulizi wa kitabu* | Karibu nyaraka zote zinao utangulizi | Tekeleza kwa kuonyesha yale utakayotenda uliojifunza<br>**-Mtatenda nini?**<br>**-Utatendaje?** |
| Mst 1 Paulo na Timotheo | Paulo ndiye mwandishi wa kifungu hiki lakini anahushisha jina la Timotheo; | |
| Mtumishi wa Yesu Kristo | Paulo anatambua ya kuwa yu hai kumtumikia Yesu | Mimi/sisi tunataka kumtumikia Yeus Kristo. Tutafanya nini?<br>1. Kuzaa nia ya utumishi<br>2. Fundisha shule ya Jumapili<br>3. Jitoa kusaidia kanisani |
| Kwa watenda katika Yesu Kristo | Paulo anawaandikia walioamini. Mtakatifu si sanamu bali ni mtu aliyezaliwa mara ya pili | Mimi ni mtakatifu kwa sababu Yesu yuko maishani mwangu. Kwa hivyo nitaishi kitakatifu kwa maisha ya Kikristo. |
| Mst 2 Amani na Neema | Maneno yaliyotumika katika kusalimiana na yamo katika nyaraka zote za Paulo.<br>Neema – kibali cha Mungu<br>Amani – uhuru mbali na hofu na fedheha mioyoni mwetu | Nina neema na amani ya Mungu katika maisha yangu. Haipasa mimi niishe kwa hofu. Neema na amani yainisha maisha yangu |
| **2.) Wazo Mst 3-6**<br>*Hii mistari ni ya kujumlisha kusudi la barua hii.* | | |
| Mst 4 Maombi na Furaha | Paulo anayofuraha si kwa sababu ya hali iliyo mazingira bali ni kazi ya Kristo maishani mwake. | Ninaweza kufurahi licha ya mazingira yangu kwa ajili ya kazi ya Kristo maishani mwangu |

# Zoezi: 2

1. Soma Zaburi sura ya kwanza (1) mara zaidi ya moja.
2. Changanua kifungu ukitumia changanuzi rahisi.
3. Unda chanzo cha kifungu kwa kutumia uchanganuzi.

# Zaburi 1

1) Heri mtu yule asiyekwenda Katika shauri la wasio haki: Wala hakusimama katika njia ya wakosaji; Wala hakuketi barazani pa wenye mizaha.

2) Bali sheria ya BWANA ndiyo impendezayo, Na sheria yake huitafakari mchana na usiku.

3) Naye atakuwa kama mti uliopandwa, Kandokando ya vijito vya maji, Uzaao matunda yake kwa majira yake, Wala jani lake halinyauki; Na kila alitendalo litafanikiwa.

4) Sivyo walivyo wasio haki; Hao ni kama makapi yapeperushwayo na upepo.

5) Kwa hiyo wasio haki hawatasimama hukumuni, Wala wakosaji katika kusanyiko la wenye haki.

6) Kwa kuwa BWANA anajua njia ya wenye haki, Bali njia ya wasiohaki itapotea.

# Waraka

Katika zoezi hili utachunguza waraka ukitumia vifaa vya msingi kufaharisi na kuchanja. Rejelea mambo uliojifunza ya ufaharisi na uchanjaji (uk 18-21).

## Zoezi: 3

1. Soma kifungu (Yuda) mara kadhaa.
2. Changanua kifungu ukitumia faharasa ya nyaraka (kama ilivyoonyeshwa, ukurasa 20).
3. Gawa kifungu kama (ilivyonyeshwa ukurasa wa 21).

# YUDA

1) Yuda, mtumwa wa Yesu Kristo, ndugu yake Yakobo, kwa hao walioitwa walipendwa katika Mungu Baba, na kuhifadhiwa kwa ajili ya Yesu Kristo.

2) Mwongezewe rehema na amani na upendano.

3) Wapenzi nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu.

4) Kwa maana kuna watu waliojiingiza kwa siri, watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, makafiri, wabadilio neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi, nao humkana yeye peke yake Mola, na Bwana wetu Yesu Kristo.

5) Tena napenda kuwakumbusha, ijapokuwa mmekwisha kujua haya yote, ya kwamba Bwana, akiisha kuwaokoa watu katika nchi ya Misri, aliwaangamiza baadaye wale wasioamini.

6) Na malaika wasiolinda enzi yao wenyewe, lakini waliyaacha makao yao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu.

7) Kama vile Sodoma na Gomora, na miji iliyokuwa kando-kando, waliofuata uasherati kwa jinsi moja na hawa, wakaenda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili, imewekwa kuwa dalili, wakiadhibiwa katika moto wa milele.

8) Kadhalika na hawa, katika kuota kwao, huutia mwili uchafu, hukataa kutawaliwa na kuyatukana matukufu.

9) Lakini Mikaeli, malaika mkuu, aliposhindana na Ibilisi, na kuhojiana naye wa ajili ya mwili wa Musa, hakuthubutu kumshitaki kwa kumlaumu, bali alisema, Bwana na akukemee.

10) Lakini watu hawa huyatukana mambo wasioyajua, na mambo wayatambuayo kwa asili wajiharibu kwayo kama wanyama wasio na akili.

11) Ole wao! Kwa sababu walikwenda katika njia ya Kaini, na kulifuata kosa la Balaamu pasipo kujizuia kwa ajili ya ujira, nao wameangamia katika maasi ya Kora.

12) Watu hawa ni miamba yenye hatari katika karamu zenu za upendo walapo karamu pamoja nanyi, wakijilisha pasipo hofu; ni mawingu yasiyo na maji, yachukuliwayo na upepo; ni miti iliyopukutika, isiyo na matunda, iliyokufa mara mbili, na kung'olewa kabisa;

13) Ni mawimbi ya bahari yasiyozuilika, yakitoa aibu yao wenyewe kama povu; ni nyota zipoteazo, ambao weusi wa giza ndio akiba yao waliowekewa milele.

14) Na Henoko mtu wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hao, akisema, Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu kwa maelfu,

15) Ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibisha wote wasiomcha Mungu, kwa ajili ya kazi zao zote za upotevu walizozitenda bila kumcha Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu yote ambayo hao wenye dhambi wasiomcha Mungu wameyanena juu yake.

16) Watu hawa ni wenye kunung'unika, wenye kulalamika, waendao kwa tamaa zao, na vinywa vyao vyanena maneno makuu mno ya kiburi, wakipendelea watu wenye cheo kwa ajili ya faida.

17) Bali ninyi, wapenzi, yakumbukeni maneno yaliyonenwa zamani na mitume wa Bwana wetu Yesu Kristo.

18) Ya kwamba waliwaambia ya kuwa, Wakati wa mwisho watakuwako watu wenye kudhihaki, wakizifuata tamaa zao wenyewe za upotevu.

19) Watu hao ndio waletao matengano, watu wa dunia hii tu, wasio na Roho.

20) Bali ninyi, wapenzi mkijijenga juu ya imani yenu iliyo takatifu sana, na kuomba katika Roho Mtakatifu.

21) Jilindeni katika upendo wa Mungu, huku mkingojea rehema ya Bwana wetu Yesu Kristo, hata mpate uzima wa milele.

22) Wahurumieni wengine walio na shaka.

23) Na wengine waokoeni kwa kuwanyakua katika moto; na wengine walihurumieni kwa hofu, mkilichukia hata vazi lililotiwa uchafu na mwili.

24) Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu.

25) Yeye aliye Mungu pekee, Mwokozi wetu kwa Yesu Kristo Bwana wetu, utukufu una yeye, na ukuu, na uwezo, na nguvu, tangu milele, na sasa, na hata milele. Amina.

# ZOEZI: 4

1. Soma kifungu (Zaburi 139) mara tena.
2. Changanua kifungu ukitumia mifano rahisi.
3. Gawanya kifungu.
4. Eleza aina ya mfanano inayotumika. Mfanano zaidi ya aina moja zinazoweza kupatikana katika kifungu kimoja (Angalia ukurasa 29 kwa maelezo zaidi).

# MASHAIRI YA KIEBRANIA

## I. MWONGOZO: TUMIA MIFANANO YA USHAIRI WA KIEBRANIA KUPATA MAANA YA KIFUNGU

A. Mashairi yamejaa lugha ya mifano, kwa hivyo lazima tujifundishe kufahamu maana ya lugha isiyo halisi au ya "picha"

B. Alama inayobainisha ushairi wa Kiebrania ni uambatanisho wa mawazo (mfanano) kati ya mstari mmoja na ule unaofuata au sehemu moja na ile inayofuata (ANGALIA: sehemu ya uchanganuzi).

C. Ushairi wa Kiebrania umetumia marudiorudio. Hayo ni ya umuhimu mkuu katika kufahamu maana yake.

**II. AINA TATU ZA MSINGI ZA MARUDIORUDIO YA MAWAZO ZA USHAIRI WA KIEBRANIA.**

A. **MFANANO FANANISHI** – Dondoo yaweza kuletwa mara ya pili au ya tatu katika njia inayokaribiana.

MFANO: Sikieni sayti yangu … sikilizeni usemi wangu Mwanzo 4:23

Unioshe … unitakase Zaburi 51:2

**B. RUDUFU YA NYONGEZI** – Mshairi huongeza kwa lile wazo la kwanza.

MFANO: ZABURI 1:1

Kila semi katika mstari inaongezea juu ya wazo la awali. Kuenenda njiani pa wasio haki ni hatua ya kwanza; kusimama pamoja na wenye dhambi ni kuzidi ubaya; na kukaa pamoja na wenye mzaha ni jumia ya ubaya wote.

**C. RUDUFU YA BAINISHI**: Mshairi akibainisha wazo moja na lingine.

MFANO: Ulimi wa mwenye hekima hutamka maarifa vizuri; bali vinywa vya wapumbavu humwaga upumbavu (Methali 15:2)

Usemi wapili kwa kawaida huleta kinyume cha wazo katika usemi wa kwanza.

# ZABURI 139

1) Ee Bwana, umenichunguza na kunijua.

2) Wewe wajua kuketi kwangu na kuondoka kwangu; Umelifahamu wazo langu tokea mbali.

3) Umepepeta kwenda kwangu na kulala kwangu, Umeelewa na njia zangu zote.

4) Maana hamna neno ulimini mwangu Usilolijua kabisa, BWANA.

5) Umenizingira nyuma na mbele, Ukaniwekea mkono wako.

6) Maarifa hayo ni ya ajabu, yanishinda mimi, Hayadirikiki, siwezi kuyafikia.

7) Nienda wapi nijiepushe na roho yako? Niende wapi niukimbie uso wako?

8) Kama ningepanda mbinguni, Wewe uko; Ningefanya kuzimu kitanda changu, Wewe uko.

9) Ningezitwaa mbawa za asubuhi, Na kukaa pande za mwisho za bahari;

10) Huko nako mkono wako utaniongoza, Na mkono wako wa kuume utanishika.

11) Kama nikisema, hakika giza litanifunika, Na nuru inzungukayo ingekuwa usiku;

12) Giza nalo halikufichi kitu, Bali usiku huangaza kama mchana; Giza na mwanga kwako ni sawasawa.
13) Maana Wewe ndiye uliyeniumba mtima wangu, Uliniunga tumboni mwa mama yangu.

14) Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa Kwa jinsi ya ajabu ya kutisha. Matendo yako ni ya ajabu, Na nafsi yangu yajua sana,

15) Mifupa yangu haikusitirika kwako, Nilipoumbwa kwa siri, Nilipoungwa kwa ustadi pande za chini za nchi;

16) Macho yako yaliniona kabla sijakamilika; Chuoni mwako ziliandikwa zote pia,

17) Mungu, fikira zako zina thamani nyingi kwangu; Jinsi ilivyo kubwa jumla yake!

18) Kama ningezihesabu ni nyingi kuliko mchanga; Niamkapo nikali pamoja nawe.

19) Ee Mungu, laiti ungewafisha waovu! Enyi watu wa damu ondokeni kwangu;

20) Kwa maana wakuasi kwa ubaya, Adui zako wakutaja jina lako bure.

21) Je! Bwana nisiwachukie wanaokuchukia? Nisikirihike nao wanaokuasi?

22) Nawachukia kwa ukomo wa chuki, Wamekuwa adui kwangu.

23) Ee Mungu unichunguze uujue moyo wangu, Unijaribu, uyajue mawazo yangu;

24) Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, Ukaniongoze katika njia ya milele.

# ZOEZI: 5

1. Soma kifungu (Mark 6:45 – 52) Zaidi ya mara moja.
2. Gawanya habari.
3. Jaribu kuuliza maswali mengi iwezekanavyo ya uchunguzaji ufafanuzi na utekelezaji, halafu uangalie ni yapi yatakayowasaidia wahusika kupitia kifungu kwa njia ya utaratibu. Ni muhimu kuuliza maswali yatakayo leta mtiririko mzuri katika kifungu.
4. Andika maswali yako kufuatana na utakavyouliza. Kando ya kila swali weka, alama (CHU) kwa uchunguzaji, (FAF) kwa ufafanuzi na (UTE) kwa utekelezaji.
5.

# Kuunda Maswali ya Kushawishi

**U**napojifunza kuandika maswali ya kujizoesha, unajifunza ujuzi. Kama utendaji wa aina zote, ujuzi wako wa kutengeneza maswali utaongezeka unapofanya kazi. Hatua kuu ya kwanza iliyo bora ni kufululiza uchunguzi wa kifungu kwa mtindo mojawapo. Kwa njia ya maswali yako, kikundi cha Biblia kitagundua uliyoyapata. Uchunguzi wa juu juu huleta maswali na mjadala hafifu bali uchunguzi sawasawa utawafanya wahusika kukabili kweli zilizo katika fungu wakielekezwa kwa Mungu na njia zake. Matokeo ya aina hii yastahili muda na bidii ya uchunguzi kwa uangalifu.

I. Soma ukijifikiria mwenyewe kwanza: Je Mungu anataka kunifundisha nini? Kisha fikiria juu ya wenzako, tutafaidi nini katika maisha yetu tunaposoma pamoja?

II. Unapomaliza kujifundisha, angalia chanzo chako na uweke alama mambo muhimu utakayohakikisha yamehusishwa.

III. Kutengeneza Maswali.

Maswali yako yahitaji kuongoza kikundi kwenye wazo kuu la fungu ili watambue mambo muhimu na wayatekeleze maishani mwao. Ni ya muhimu kukumbuka aina ya kikundi kinachofanya masomo haya; waumini, wachanga, waliokomaa zaidi, vijana, wazee n.k. Kikundi hakiwezi kwenda katika kudadisi jinsi ulivyofanya; maswali yako yatachukulia mambo ya msingi n.k. uliopata katika matayarisho uliyofanya.

A. Anza kipindi kwa maswali wafahamishe yote yaliyo katika fungu zima. (Ni nani ananenewa? Wapi? Ni nini wanachofanya? n.k.).
B. Kwa maswali waongoze kutoka mwanzo hadi mwisho wa fungu kwa utaratibu. Labda ungependa kuwafundisha sehemu kwa sehemu, mnapoendelea, wafikishe kujua jinsi beti zinavyoungana.

**C.** Utataka kuuliza **Maswali ya Uchunguzaji (mambo ya kweli.)**
**Maswali kuhusu Ufafanuzi (maana)**

**Maswali ya Utekelezi (utendaji).**

1. **Maswali ya Uchunguzaji.**
   - Kikundi kitahitaji kuona yaliyomo.
   - Kwa njia tofauti acha kikundi kione **nani, nini, lini, wapi**.
   - Wanaweza kusimulia baadhi ya watu au matukio.
   - Wasaidie kuingia "katika" tukio, wahusishe kisa na mazungumzo au wafanye igizo kuhusu Efeso ya karne ya kwanza, wakiupokea waraka wa mtume Paulo.
   - Ongoza kikundi katika kufahamu muundo uliyoupata: Ni nini tofauti kati ya uchunganuzi na utendaji.
2. **Maswali ya Uchambuzi**
   - Peleka kikundi katika kufafanua na kuuliza kwa nini ili wazipate kweli kuu.
   - Watahitaji ufafanuzi wa semi na maneno.
   - Wasaidie kuona sababu iliyo nyuma ya miundo (uliza maswali yanayotokana na ufafanuzi wako). Hii ni njia ya kuwaonyesha muungano wa beti tofauti).
   - Wanapoipata kweli kuu maswali yako yatakuwa ya kuwasaidia kuelewa.

3. **Maswali ya Utekelezi (Utendaji)**
   - Haya maswali hufanya kikundi kufikiria na kufanya mabadiliko katika maisha – nia, uhusiano na matendo yao.
   - Maswali ya utendaji yanahitaji kutiririka kutoka kwa maana ya mawazo kuu na yanatokea baada ya mawazo hayo kueleweka. Kumbuka kuwa ni jambo kuwa na maswali machache ya aina hii katika sehemu mbali mbali za fungu kuliko mengi.

# Marko 6:45–52

45) Mara akawalazimisha wanafunzi wake wapande mashuani, watangulie kwenda ng'ambo hata Bethsaida wakati yeye alipokuwa akiwaaga mkutano.

46) Hata alipokwisha kuagana nao akaenda zake mlimani kuomba.

47) Na kulipokuwa jioni, mashua ilikuwa katikati ya bahari, na yeye yu peke yake katika nchi kavu.

48) Akawaona wakitaabika kuvuta makasia, kwa maana upepo ulikuwa wa mbisho; hata ilipopata kama zamu ya nne ya usiku akawaendea, akitembea juu ya bahari, akataka kuwapita.

49) Nao walipomwona akitembea juu ya bahari, walidhani ya kuwa ni kivuli, wakapiga yowe.

50) Kwa kuwa wote walimwona, wakafadhaika. Mara akasema nao, akawaambia, Changamkeni, ni mimi, msiogope.

51) Akapanda mle chomboni walimo; upepo ukakoma; wakashangaa sana mioyoni mwao.

52) Kwa maana hawakufahamu habari za ile mkate, kwa sababu mioyo yao ilikuwa mizito.

# Kutengeneza chanzo cha maswali ya Kuzoeza.

Kutokana na chanzo ulichotengeneza, kuza maswali kutoka kila aya. Hii kazi hasa ni ya 'kujibu' maswali yako. Kwa maneno mengine, habari zilizomo katika aya zinapaswa kuenda pamoja na maswali uliyoandika.

**Kuza maswali ya uchunguzaji kutoka katika ubeti wake maswali ya ufafanuzi na maswali ya utendaji vile vile**

| "**Uch**" Uchunguzaji | "**Ufa**" Ufafanuaji | "**Ute**" Utekelezaji |
|---|---|---|
| Wazo: 1 -<br>Mst 1 - uchunguzaji<br>- uchunguzaji<br>- uchunguzaji<br><br>Mst 2 - uchunguzaji<br>- uchunguzaji<br><br>Wazo: 2 -<br>Mst 3 - uchunguzaji<br>n.k. | Fafanuzi za uchunguzi hapa<br>- fafanuzi<br>- fafanuzi | Utendaji hapa.<br>- Nifanye nini?<br>- Nifanyeje?<br>(Toa mifano) |

**<u>Juu ya kuuliza na maswali</u>**

Orodhesha maswali taratibu k.v. ukiyakuza kutoka kwa chanzo na kifungu tayari.

Maswali yawe rahisi, safi ya kupeleka watu kwenye fungu kwa majibu.

Maswali yalete mjadala unaokuza ufahamu wa fungu.

Maswali yanapaswa kuwa na mtiririko took wazo moja hadi lingine

Maswali yaweza kujibika katika fungu yaani uweze kujibu swali lako

(Separate Sheet of Paper)

## Orodha ya maswali kutoka chanzoni.

Wazo 1 la Faharasa/chanzo.

**Uch** 1. Uchunguzi (Ni nani aliyehusika, walifanya nini n.k.?)
**Uch** 2. Uchunguzi (Walikuwa wapi?)
**Uch** 3. Uchunguzi (Nini kilitokea?)

*(Baada ya maswali machache uliza maswali mawili au moja ya ufafanuzi.)*

**Ufa** 4. Ufafanuzi (Yesu alisema nini?)
**Ufa** 5. Ufafanuzi (Paulo alimaanisha nini aliposema…?)

*(Baada ya maswali haya ni vyema kuuliza maswali ya utendaji yanatokana na majibu yake.)*

**Ute** 6. Maswali ya utendaji (Majibu no orodha ya vitendo ya kutenda k.v. Nitafanya nini nipate kuwa kama Yesu?)
**Ute** 7. Maswali ya matendo (Nitachukua hatua gani?)

*(Endeleza kufanya kazi hii ukitumia chanzo chako kwa fungu lote, wazo kwa wazo, mstari kwa mwingine..)*

Kila swali yafaa kuwa "UCH", "UFA", ama "UTE" (kama kwenye somo la 5)

# Zoezi: 6

1. Soma fungu (Marko 4: 1 – 20) mara kadhaa.

2. Faharisi fungu kwa faharasa rahisi.

3. Pata dondoo kuu inayosisitizwa katika mfano.

4. Chanja kifungu ukitumia Faharasa. Uwe makini wa kufafanua mfano ukitumia maelezo ya kifungu (yakiwemo).

5. Tayarisha maswali yako ya uchunguzi, ufafanuzi na utendaji.

# Mifano (Ya Yesu)

**M**fano ni hadithi fupi inayotumia mfano halisi ya maisha ya kila siku kuonyesha ukweli wa kiroho. Yesu mara nyingi alifundisha kwa mifano na ni ya muhimu sana sisi kufahamu ufasaha huu wa kipekee. Yesu alipofundisha kwa mifano alikuwa na kusudi la ziada. Alitaka kuuficha ule ukweli mbali na watu waliokataa wito, huku akiweka wazi mbele yao wanaoitikia.

Angalia kwamba, ingawa matukio ya historia yanaweza kupata matamshi ya kuonyesha, mifano ya Yesu ilikuwa hadithi maalum zilizoundwa kwa kusudi la kufundisha ukweli fulani. Ingawa kwa ufafanuzi wake, mfano si nakala ya matukio ya historia, na kuwa mfano ni lazima uwe kwa maisha ya kila siku.

# KUNA MAMBO MANNE YANAYOHITAJIKA KATIKA KUFAHAMU MIFANO.

**1. Anza na yaliyomo ndani ya kifungu:**

a) Ni hali gani inayoleta usimulizi wa hadithi hii (Lk 15:1 – 2)

b) Ni maelezo gani ya maana ya mfano? (Lk 15:7 na 10)

**2. Tambua jambo kuu linalosisitizwa:**

Angalia yaliyomo kifunguni kabla na baada ya mfano.

a) Luka 15:4 Kondoo mmoja aliyepotea

b) Luka 15:8 – 10 Sarafu moja iliyopotea.

**3. Tambua jambo lisilomuhimu**

Mambo ambayo hayatumiki kufundisha ukweli.

a) Luka 15:4 Kondoo 99 salama.

b) Luka 15:8 Sarafu 9 salama

**4. Tambua jambo muhimu**

Mambo ambayo makusudi yake ni kufundisha ukweli. Fulani, yatakayojengwa kwenye dondoo kuu (mwana mpotevu – alipotea bali sasa amepatikana).

# MARKO 4:1-20

1) Akaanza kufundisha tena kando ya bahari. Wakamkusanyikia mkutano mkubwa mno, hata yeye akapanda chomboni, akakaa baharini; mkutano wote ulikuwako juu ya nchi kavu kando ya bahari.
2) Akawafundisha mambo mengi kwa mifano, akawaambia katika mafundisho yake,
3) Sikilizeni; Tazama mpanzi alitoka kwenda kupanda;
4) Ikawa alipokuwa akipanda, mbegu nyingine ilianguka kando ya njia, wakaja ndege wakaila.
5) Nyingine ikaanguka penye mwamba, pasipokuwa na udongo mwingi; mara ikaota kwa kuwa na udongo haba;
6) Hata jua lilipozuka iliungua, na kwa kuwa haina mizizi ikanyauka.
7) Nyingine ikaanguka penye miiba; ile miiba ikamea, ikaisonga, isizae matunda
8) Nyingine ikaanguka penye udongo ulio mzuri, zikazaa matunda, zikamea na kukua, na kuzaa, moja thelathini, moja sitini, na moja mia.
9) Akasema, aliye na masikio ya kusikilia, na asikie.
10) Naye alipokuwa peke yake, wale watu waliomzunguka, na wale Thenashara, walimwuliza habari za ile mifano.
11) Akawaambia, Ninyi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu, bali kwa wale walio nje yote hufanywa kwa mifano,
12) ILI WAKITAZAMA WATAZAME, WASIONE;
NA WAKISIKIA WASIKIE, WASIELEWE; WASIJE WAKAONGOKA, NA KUSAMEHEWA.

13) Akawaambia, Hamjui mfano huu? Basi mifano yote mtaitambuaje?
14) Mpanzi huyo hulipanda neno.
15) Hawa ndio walio kando ya njia, lipandwapo neno; nao wakiisha kusikia, mara huja Shetani, akaliondoa lile neno lililopandwa mioyoni mwao.
16) Kadhalika na hawa ndio wapandwao penye miamba, ambao kwamba wakiisha kulisikia lile neno, mara hulipokea kwa furaha;
17) Ila hawana mizizi ndani yao, bali hudumu muda mchache; kasha ikitokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara hujikwaa.
18) Na hawa ndio wale wapandwao penye miiba; ni watu walisikiao lile neno,
19) Na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali, na tamaa za mambo mengine zikiingia, hulisonga lile neno, likawa halizai.
20) Na hawa ndio waliopandwa penye udongo ulio mzuri; ni watu walisikiao lile neno na kulipokea, na kuzaa matunda mmoja thelathini, mmoja sitini, na mmoja mia.

# Zoezi: 7

1. Soma kifungu (Isaya 1:1- 31) urudie mara tena.
2. Fahirisi kifungu (tumia faharasa rahisi).
3. Pambanua aina ya unabii wa kila wazo katika faharasa.
4. Pata kumcha nabii.
5. Chanja kifungu ukitumia faharasa uliyotayarisha.
6. Tayarisha faharasa ya mahubiri utakayotumia kufafanua kifungu. Chukua wazo la kwanza na ulijengee mstari juu ya mstari. Sema wazo linalotangulia a ufafanue kila mstari unaochangia. Huenda utahitaji kufafanua maneno na semi katika kifungu ulichunguza fafanua na kutekeleza. Enenda kwenye wazo linalofuata ulijenge nalo pia. Fikiria hadithi na onyesho linaloweza kutumika kuleta wazo hilo.

# Unabii

## Unabii unapatikana katika Biblia tangu Mwanzo mpaka Ufunuo.

- Katika idadi ya mistari 23,210 ya Agano la Kale, mistari 6,641 (karibu 28%) ni mambo ya utabiri.
- Katika idadi ya mistari 7,194 ya Agano Jipya, mistari 1,711 (karibu 21%) ni mambo ya utabiri.
- Kwa hiyo, katika idadi ya mistari 32,124 ya Biblia nzima, mistari 8,352 (karibu 27%) ni mambo ya utabiri.

Ikiwa katika maandiko yanapatikana mambo mengi hivi ya utabiri, inamaanisha ya kwamba unabii umepewa nafasi muhimu na Mungu.

I. Hatua ya kwanza ya Mwanafunzi wa Biblia yeyote yule ni kutambua aina ya unabii anaosoma.

**Kuna aina mbili za unabii:**

A. **UTABIRI –** usemao mambo yatakayotokea wakati wa usoni na

B. **BUSARA –** unaohusu itikadi, maadili na elimu ya Mungu

Baadhi ya unabii umechanganya hayo mawili. Katika Zekaria 1:1 – 15 ni wa busara bali maoni yanayofuata ni utabiri (1:16 – 21). Sehemu kubwa ya Zekaria 7 ni ya busara, bali sehemu zinazotangulia na zinazofuata ni utabiri. Unabii, hata hivyo, ni utabiri kwa wingi.

II. Haya ni baadhi ya maelekezo ya kujifunza unabii na utabiri.

**A. LUGHA HALISI –** kabili kifungu kwa maana yake iliyo rahisi, ya moja kwa moja na kawaida ikiwa hakuna sababu ya kufanya lingine. Mstari ya utabiri imepaswa kuchukuliwa jinsi ilivyo kama hakuna sababu ya kuelewa kama mfano. Kila mara angalia maana rahisi ya moja kwa moja, yaani unavyonena ndivyo anavyomaanisha.

**B. LUGHA FANANISHI**. Jifunze kutambua mafungu yenye mifano, lakini ufuate masharti ya kawaida ya kutofuatisha kati ya lugha rahisi na ya mifano.

1. Baadhi ya lugha ni ya mifano na kuhalisisha ni dinikozo. Kwa mfano Yoeli 2:31 – mwezi ukigeuka kuwa damu; Isaya 11:1 shina linalotoka katika mwanadamu; Zekaria 4:7 – mlima ukiondoshwa.
2. Haya maonyesho tutayaita “lugha ya picha”, jinsi tuonavyo katika Danieli, simba mwenye mbawa, chui mwenye mabawa manne n.k.
3. Lengo hasa ni kupambanua yanayoainishwa na picha, kwa sababu kile kitu kinachoonyeshwa kwenye picha kitatukia kihalisi katika historia. Mfano: Danieli 7:17 – wale wanyama wanne walimaanaisha wafalme wanne watakao inuka duniani; Yohana 2:19 utabiri wa Yesu wa hekalu,” nitaliharibu hili hekalu na katika siku tatu kuliinua tena,” maelezo yake ni Kristo anasema juu ya hekalu la mwili wake.

**C. TAHADHARI**

Kutambua aina ya unabii katika baadhi ya mafungu ni vigumu.

Mfano: Amosi 9:13 – 15. Kuna alama ya kuwa fungu hili ni picha. Lakini lazima tuanze kuchukulia utabiri kuwa halisi. Utabiri huu kwa wingi ni picha na inatupasa kujifunza kutofautisha kati ya hayo mawili.

D. Unabii unahusu yaliyopita, yaliyopo na yajayo. Mara kwa mara unabii haufuati mpangilio wa mawazo. Kifungu huweza kuruka toka wazo moja hadi lingine, au toka wakati mmoja hadi mwingine.

# ISAYA 1:1 –31

1) Haya ni maono ya Isaya, mwana wa Amozi, aliyoyaona katika habari za Yuda na Yerusalemu, siku za Uzia na Yothamu na Ahazi na Hezekia, wafalme wa Yuda.

2) Sikieni enyi mbingu, tega sikio, Ee nchi, wa maana BWANA amenena. Nimewalisha watoto na kuwalea, nao wameniasi.

3) Ng'ombe amjua bwana wake

Na punda ajua kibanda cha bwana wake.

Bali Israeli hajui, watu wangu hawafikiri.

4) Ole wake, taifa lenye dhambi, watu wanaochukua mizigo ya uovu, wazao wa watenda mabaya, watoto wanaoharibu, wamemwacha BWANA, wamemdharau yeye aliye Mtakatifu wa Israeli, wamefarakana naye na kurudi nyuma.

5) Mbona mnataka kuigwa hata sasa, hata mkazidi kiasi? Kichwa chote ni kigonjwa, moyo wote umezimia.

6) Tangu wayo wa mguu hata kichwani hamna uzima ndani yake, bali jeraha na machubuko na vidonda vitokavyo usaha; havikufungwa, havikuzongwa-zongwa, wala havikulainishwa kwa mafuta.

7) Nchi yenu ni ukiwa, miji yenu imeteketezwa kwa moto; nchi yenu, wageni wameila mbele ya macho yenu, nayo ni ukiwa, kana kwamba imeangamizwa na wageni.

8) Na binti Sayuni ameachwa kama kibanda katika shamba la mizabibu, kama kipenu katika shamba la matango, kama mji uliohusuriwa.

9) Kama BWANA wa majeshi asingalituachia mabaki machache sana, tungalikuwa kama
Sodoma, tungalifanana na Gomora.

10) Lisikieni neno la BWANA enyi waamuzii wa Sodoma, tegeni masikio msikie sheria ya Mungu wetu, enyi watu wa Gomora.

11) Huu wingi wa sadaka zenu mnazonitolea una faida gani? Asema BWANA, Nimejaa mafuta ya kafara za kondoo waume, na mafuta ya wanyama walionona; nami siifurahi damu ya ng'ombe wala ya wana-kondoo wala ya mbuzi waume.

12) Mjapo ili kuonekana mbele zangu, ni nani aliyetaka neno hili mikononi mwenu, kuzikanyaga nyua zangu?

13) Msilete tena matoleo ya ubatili; uvumba ni chukizo kwangu; mwezi mpya na Sabato; kuita mkutano; siyawezi maovu hayo na makutano ya ibada.

14) Sikukuu zenu za mwezi mpya na karamu zilizoamriwa, nafsi yangu yazichukia; mambo hayo yanilemea; nimechoka kuyachukua.

15) Nanyi mkunjuapo mikono yenu, nitaficha macho yangu nisiwaone; naam mwombapo maombi mengi, sitasikia; mikono yenu imejaa damu.

16) Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu; acheni kutenda mabaya;

17) Jifunzeni kutenda neema; takeni hukumu na haki; wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane.

18) Haya, njooni tusemezane, asema BWANA. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.

19) Kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi;

20) Bali kama mkikataa na kuasi mtaangamizwa kwa upanga; maana kinywa cha BWANA kimenena haya.

21) Mji huu uliokuwa mwaminifu umekuwaje kahaba! Yeye aliyejaa hukumu ya haki; haki ilikaa ndani yake, bali sasa wauaji!

22) Fedha yako imekuwa takataka, divai yako imechanganywa na maji.

23) Wakuu wako ni waasi, na rafiki za wevi; kila mtu hupenda rushwa hufuata malipo; hawampatii yatima haki yake, wala maneno ya mjane hayawawasili.

24) Kwa hiyo, asema Bwana, BWANA wa majeshi, Mwenye enzi, wa Israeli, Nitapata faraja kwa hao wanipigao, nitatwaa kisasi kwa adui zangu;

25) Nami nitakuelekezea wewe mkono wangu, na kukutakasa takataka zako kabisa, na kukuondolea bati lako lote;

26) Nami nitarejeza upya waamuzi wako kama walivyokuwa hapo kwanza, na washauri wako kama hapo mwanzo; baada ya hayo utaitwa, Mji wa haki, mji mwaminifu.

27) Sayuni itakombolewa kwa hukumu na waongofu wake kwa haki.

28) Lakini kuharibika kwao wakosao nao wenye dhambi kutatokea wakati mmoja, nao wamwachao BWANA watateketezwa.

29) Kwa maana watatahayarika kwa sababu ya mialoni mliyoitamani, nanyi mtaaibishwa kwa sababu ya bustani mlizozichagua.

30) Maana mtakuwa kama mwaloni ambao majani yake yakauka na kama bustani isiyo na maji.

31) Na mtu hodari atakuwa kama makumbi, na kazi yake kama cheche za moto; nao watawaka pamoja wala hapana atakayewazima.

## MFANO
## Changanuo ya ujumbe wa kuchambua

(Zaburi 1 kwa mfano)

- **UTANGULIZI –** Kuwavutia wasikilizaji wako na maelekezo ya ujumbe wako.

1) Toa muhtasari wa fungu k.v. mazingira, wakati n.k.
2) Eleza kiini cha fungu – ukitumia maonyesho yanayohusisha kiini hiki katika maisha ya kisasa.

**Mfano**: Hii ni Zaburi ya maelekezo iliandikwa na mshairi asiyejulikana kuhusu njia mbili za maisha…zikiwekwa kwetu kama kauli – ili tuweze kufuata njia ya haki iletayo furaha.

- **MAUDHUI –** Ndiyo moyo wa ujumbe ukifuata mchanganuo, kutoka kwenye sehemu ya "maudhui" (sehemu za uchanganuzi) kama wazo kuu. Tumia "maelezo" ya mstari mmoja au miwili katika kila sehemu ya faharasa kusisitiza wazo kuu lililotokana na uchunguzaji, ufafanuzi na utekelezaji katika vyanzo tayari. Tumia maonyesho na mifano kusanifu dondoo na kuipatanisha na wazo kuu (kiini). Angalia mfano (rudi kwa majibu ya Zaburi 1).

I. **Amebarikiwa mtu yule** mst 1 – 3: Mistari hii inaeleza juu ya mtu mtumwa (jinsi alivyo, anavyotenda na anavyofanyika kuwa. Mst 1 yeye "amebarikiwa" yaani mwenye ujuzi wa furaha ya kweli (ndani, rohoni), "asiyekwenda…hakusimama…hakuketi hujiepusha na vikundi vya watenda maovu (mfano hasa wa marudiorudio ya kiebrania) na badala yake yeye hupendezwa na neno. Yeye ni kama mti uliopandwa kando kando ya vijito vya maji, kuleta picha ya aina ya lishe ni ufanisi Mungu anaowapa watu wake.

II. **Mtu asiyehaki** mst 4 – 6: Sivyo walivyo wasio haki yaani mambo yanayohusu watu wasio watauwa mst 4. Hawapendezwi na sheria ya BWANA. Huku watauwa wakiwa kama miti ya Matunda iliyoona dhamani, wasio haki ni kama makapi. Yapeperushwayo kwa upepo, yasiyo na thamani katika hesabu ya Mungu.
Mst 5 – 6 tunasoma juu ya masaibu yatakayowapata wasio haki mbali na maisha ya msomi ya mwishoni ya wenye haki.

- **KUMALIZA:** Hapa ujumbe wetu unakaribia mwisho kwa kuchanganya mawazo yote katika kiini na mafunzo tukitekeleza kwa ujumla wake kwa kutumia mifano na maelekezo vile vile ilivyosemwa na kufundishwa katika ujumbe.

**Mfano**: Hebu tupate kuwa na shauku ya neno la Mungu, na baraka anazopata mwenye haki zituhimize kumtafuta Mungu, kushiriki ana neno lake pamoja na hao waliopotea n.k.

**ANGALIA:** Mawazo yote, au dondoo kuu, maudhui ya mistari mifano na maonyesho yanapaswa kuhusiana na kiini – kusisitiza na kufanya ionekane kwa urahisi na kwa jinsi ya kueleweka.

# Kazi ya Mazoezi Level 3

# Zoezi: 8

1. Soma mistari (Yohana 13:1-20) mara nyingi (soma mara tatu).

2. Jibu maswali ya Kuhusisha Ukurasa wa 46.

# Yohana 13:1-20

1) Basi, kabla ya Sikukuu ya Pasaka Yesu, hali akijua ya kuwa saa yake imefika, atakayotoka katika ulimwengu kwenda kwa Baba, naye ali amewapenda watu wake katika ulimwengu, aliwapenda upeo.
2) Hata wakati wa chakula cha jioni, naye Ibilisi amekwisha kumtia Yuda, mwana wa Simoni Iskariote, moyo wa kumsaliti.
3) Yesu, hali akijua ya kuwa Baba amempa vyote mikononi mwake, na ya kuwa alitoka kwa Mungu naye anakwenda kwa Mungu.
4) Aliondoka chakulani, akaweka kando mavazi yake, akatwaa kitambaa, akajifunga kiunoni.
5) Kisha akatia maji katika bakuli, akaanza kuwatawadha wanafunzi miguu, na kuifuta kwa kile kitambaa alichojifunga.
6) Hivyo yuaja kwa Simoni Petro. Huyo akamwambia, Bwana! Wewe wanitawadha mimi miguu?
7) Yesu akajibu, akamwambia, Nifanyalo wewe hujui sasa, lakini utalifahamu baadaye.
8) Petro akamwambia, wewe hutanitawadha miguu kamwe. Yesu akamwambia, Kama nisipokutawadha , huna shirika nami.
9) Simoni Petro akamwambia, Bwana, si Miguu yangu tu, hata na mikono yangu na kichwa changu pia.
10) Yesu akamwambia, yeye aliyekwisha kuoga hana haja ila ya kutawadha miguu, bali yu safi mwili wote, nanyi mmekuwa safi, lakini si nyote.
11) Kwa maana alimjua yeye atakayemsaliti, ndiyo maana alisema, si nyote mlio safi.
12) Basi alipokwisha kuwatawadha miguu, na kuyatwaa mavazi yake, na kuketi tena, akawaambia, Je! Mmeelewa na hayo niliyowatendea?
13) “Nyinyi mwaniita, Mwalimu, na Bwana, nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo”.
14) “Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi.
15) “Kwa kuwa nimewapa kielelezo, ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo.”
16) Amini amini, nawaambia ninyi, mtumwa si mkuu kuliko Bwana wake, wala Mtume si mkuu kuliko yeye aliyempeleka.
17) “Mkiyajua hayo heri ninyi mkiyatenda.”
18) “Sisemi habari za ninyi nyote, nawajua wale niliowachagua, lakini andiko lipate kutimizwa. Aliyekula chakula changu, ameniinulia kisigino chake.
19) “Tangu sasa nawaambia kabla hayajatukia, ili yatakapotukia mpate kuamini ya kuwa mimi ndiye.
20) “Amini, Amini, nawaambieni, yeye ampokeaye mtu yeyote nimpelekaye, anipokea mimi, naye anipokeaye mimi ampokea yeye aliyenipeleka.

# Maswali ya Kuhusisha

**Uch** 1. Ni nani hao watu waliohusika kwenye hii hadithi?

**Uch** 2. Ni tukio gani lililota kutokea?

**Ufa** 3. Karamu ya Pasaka ni nini?

**Uch** 4. Elezea kwa maneno yako mwenyewe matukio ya kifungu hiki.

**Uch** 5. Yesu alijua nini kumhusu yeye mwenyewe kilicho tajwa katika mstari wa 1?

**Ufa** 6. Yesu aliwapenda wanafunzi wake kiasi gani?

**Ufa** 7. Je, Yuda Iskarioti alikuwemo katika upendo huo?

**Ufa** 8. Ilikuwaje Yesu ampende mtu ambaye baada ya muda mfupi angemsaliti?

**Uch** 9. Orodhesha mambo ambayo Yesu anayajua kumhusu yeye mwenyewe katika mstari wa 3.

**Ufa** 10. Ni kwanini Yesu aliwaosha wanafunzi miguu?

**Ufa** 11. Kwa kawaida ni kazi ya nani kuosha miguu?

**Uch** 12. Petro alilipokeaje pendo la kuoshwa miguu na Yesu?

**Ufa** 13. Kwa nini Petro hakutaka Yesu amuoshe miguu?

**Uch** 14. Petro alilipokeaje jibu la Yesu katika mstari wa 9?

**Ufa** 15. Elezea Yesu alimaanisha nini katika mstari wa10.

**Ute** 16. Wewe ungelijibuje swali la Yesu katika mstari wa12?

**Ufa** 17. Ni kwanini Yesu anasema tunatakiwa kuoshana miguu?

**Ufa** 18. Yesu alimaanisha nini kwa kauli yake katika mstari wa16?

**Ufa** 19. Ni kwanini haitoshi kujua tu mambo, (Tazama mstari wa17)?

**Ufa** 20. Yesu anamwongelea nani katika mstari wa18?

**Ufa** 21. Tafadhali fasiri mstari wa 20.

**Ute** 22a. Tafadhali tengeneza matumizi ya mafundisho makuu ya ujumbe huu.

**Ute** 22b. Nini kingekuwa matumizi ya jumla?

**Ute** 22c. Ni mambo gani mahususi unayoweza kufanya?

## Kazi ya Kuchagua #2

1. Soma mstari (Filemoni) mara nyingi.
2. Andika ufupisho wa Maandiko haya kwa kutumia fomu ya Ufipisho wa Waraka (kama ilivyoonyeshwa kwenye ukurasa wa 20).
3. Weka mistari hii kwenye Jedwali kama ilivyoonyeshwa ukurasa wa 21.

# Filemoni

1) Paulo, mfungwa wa Kristo Yesu, na Timotheo aliye ndugu yetu, kwa Filemoni mpendwa wetu, mtenda kazi pamoja nasi,

2) Na kwa Afia, ndugu yetu, na kwa Arkipo askari mwenzetu, na kwa kanisa lililo katika nyumba yako.

3) Neema na iwe kwenu, na amani, zitokanazo kwa Mungu, Baba yetu, na kwa Bwana Yesu Kristo.

4) Namshukuru Mungu siku zote, nikikukumbuka katika maombi yangu,

5) Nikisikia habari za upendo wako na imani uliyo nayo kwa Bwana Yesu na kwa watakatifu wote,

6) Ili kwamba ushirika wa imani yako ufanye kazi yake, katika ujuzi wa kila kitu chema kilicho kwetu, katika Kristo.

7) Maana nalikuwa na furaha nyingi na faraja kwa sababu ya upendo wako, kwa kuwa mioyo ya watakatifu imeburudishwa nawe, ndugu yangu.

8) Kwa hiyo, nijapokuwa nina ujasiri katika Kristo kukuagiza likupasalo,

9) lakini, kwa ajili ya upendo nakusihi, kwa kuwa ni kama nilivyo, Paulo mzee, na sasa mfungwa wa Kristo Yesu pia.

10) Nakusihi kwa ajili ya mtoto wangu niliyemzaa katika vifungo vyangu, yaani, Onesimo,

11) ambaye zamani alikuwa hakufai, bali sasa akufaa sana, wewe na mimi pia,

12) niliyemtuma kwako, yeye mwenyewe, maana ni moyo wangu hasa,

13) ambaye mimi nalitaka akae kwangu, apate kunitumikia badala yako katika vifungo vya Injili.

14) Lakini sikutaka kutenda neno lolote isipokuwa kwa shauri lako, ili kwamba wema wako usiwe kama kwa lazima, bali kwa hiari.

15) Maana, labda ndiyo sababu alitengwa nawe kwa muda, ili uwe naye tena milele,

16) tokea sasa, si kama mtumwa, bali zaidi ya mtumwa, ndugu mpendwa, kwangu mimi sana, na kwako wewe zaidi sana, katika mwili na katika Bwana.

17) Basi kama ukiniona mimi kuwa mshirika nawe, mpokee huyu kama mimi mwenyewe.

18) Na kama amekudhulumu, au unamwia kitu, ukiandike hicho juu yangu.

19) Mimi Paulo nimeandika kwa mkono wangu mwenyewe, mimi nitalipa. Sikuambii kwamba nakuwia hata nafsi yako.

20) Naam, ndugu yangu, nipate faida kwako katika Bwana, uniburudishe moyo wangu katika Kristo.

21) Kwa kuwa nakuamini kutii kwako ndiyo maana nimekuandikia, nikijua ya kuwa utafanya zaidi ya hayo nisemayo.

21) Na pamoja na hayo uniwekee tayari mahali pa kukaa, maana natarajia ya kwamba kwa maombi yenu mtajaliwa kunipata.

23) Epafra, aliyefungwa pamoja nami katika Kristo Yesu, akusalimu,

24) na Marko, na Aristarko, na Dema, na Luka, watendao kazi pamoja nami.

25) Neema ya Bwana Yesu Kristo na iwe pamoja na roho zenu.

# Kazi ya Kuchagua #3

1. Soma Maandiko (Isaya 55) mara kadhaa (mara tatu).

2. Uandike ufupisho wa Maandiko haya (tumia ufupisho rahisi).

3. Tofautisha aina za unabii katika kila wazo la huo ufupisho.

4. Tafuta wazo kuu la huu unabii.


5. Weka mistari hii kwenye jedwali ukitumia ufupisho wake.

6. Tunga ufupisho wa mahubiri ambao utatumia kufafanua maandiko haya. Chukua wazo la kwanza na kulikuza mstari kwa mstari. Taja wazo la kwanza na kuanza kuelezea kila mstari unaolihusu. Unaweza ukataka kuelezea maneno na kauli za msingi katika kifungu hicho ambayo umeyaona, ukayafasiri, na kuyatumia. Kisha endelea hadi kwenye wazo linalofuata na kulikuza. Jaribu kufikiria vielelezo na hadithi kulielezea hilo wazo. (Angalia mfano ulioko ukurasa wa 43)

# ISAYA 55

1) Haya, kila aonaye kiu, njoni majini, naye asiye na fedha, njoni, nunueni mle, naam, njoni, nunueni divai na maziwa, bila fedha na bila thamani.
2) Kwani kutoa fedha kwa ajili ya kitu ambacho si chakula, na mapatao yenu kwa kitu kisichoshibisha? Nisikilizeni kwa bidii, mle kilicho chema, na kujifurahisha nafsi zenu kwa unono.
3) Tegeni masikio yenu na kunijia, Sikieni, na nafsi zenu zitaishi, Nami nitafanya nanyi agano la milele, Naam, rehema za Daudi zilizo imara.
4) Angalieni, nimemweka kuwa shahidi kwa kabila za watu, kuwa kiongozi jemedari kwa kabila za watu.
5) Tazama, utaita taifa usilolijua, na taifa lisilokujua wewe litakukimbilia, kwa sababu ya BWANA Mungu wako, na kwa ajili yake Mtakatifu wa Israeli, maana amekutukuza.
6) Mtafuteni BWANA, maana anapatika, mwiteni maadamu yu karibu.
7) Mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake, na amrudie BWANA, naye atamrehemu, na arejee kwa Mungu wetu, naye atamsamehe kabisa.
8) Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu, asema BWANA.
9) Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.
10) Maana kama vile mvua ishukavyo, na theluji, kutoka mbinguni, wala hairudi huko, bali huinywesha ardhi, na kuizalisha na kuichipuza, ikampa mtu apndaye mbegu, na mtu alaye chakula,
11) ndivyo litakavyokuwa neno langu, litokalo katika kinywa changu, halitanirudia bure bali litatimiza mapenzi yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma.
12) Maana mtatoka kwa furaha, mtaongozwa kwa amani, mbele yenu milima na vilima vitatoa nyimbo, na miti yote ya kondeni itapiga makofi.
13) Badala ya mchongoma utamea msunobari, na badala ya mibigili, mhandesi; Jambo hililitakuwa la kumpatia Bwana jina, litakuwa ishara ya milele isiyokatiliwa mbali.

# KIAMBATANISHO



# Jinsi ya kuanzisha na kuongoza mafunzo ya Biblia

Kuanzisha mafunzo ya Biblia ni jambo la faida kubwa kwa kiongozi na washiriki. Ikiwa hujawahi kuongoza kundi kabla ya hapo, yaweza kuwa jambo la busara kuanza na kundi dogo na kuongeza idadi kidogo kidogo. Anza na mafunzo mara chache, kwa mfano mara moja kila wiki kwa mwezi mmoja. Hili litakuwezesha kujifunza kadiri unapoendelea kuwa bora zaidi. Ukianza na mafunzo marefu, watu wanaweza kupoteza hamu na kuacha kuhudhuria kabla hujapata maendeleo ya kutosha na ili linaweza kupelekea kuvunjika moyo.

## Tunatakiwa kumkaribisha nani?

Kabla hujamkaribisha mtu yeyote, tumia muda katika maombi. Ni lazima uamini kwamba Mungu anatayarisha watu wenye njaa kwa Neno lake. Ukweli wa mambo ni kwamba amekuwa akitayarisha watu kabla hata hujafikiri kuanza mafunzo! Unapoomba atawaleta watu fulani kwako ambao unajua wanatakiwa kukaribishwa. Anza na watu wachache tu, wawili au watatu wanatosha. Unapoendelea kundi litakua, lakini ni muhimu kuanza na kundi dogo.

## Ni muda kiasi gani unahitajika?

Viongozi wazoefu wa mafunzo ya Biblia wamegundua kwamba kitu chochote kinachozidi saa moja ni kirefu mno.  Baadhi ya washiriki watapoteza hamu na kuacha kuhudhuria mafunzo kama yatakuwa yanatumia muda mrefu mno. Chagua muda mzuri kukutana ambao unamfaa kila mtu, na uwe na ratiba ambayo haisumbui watu. Kuna wakati utakaa kwa muda mrefu kuliko mwingine lakini zingatia sana matakwa ya kundi lako.

# Nijitayarishaje?

Mafunzo mazuri ya Biblia "hayatokei tu yenyewe" kama ajali- yanatayarishwa kwa uangalifu. Kwanza mwache Mungu azungumze na moyo wako wakati unapojifunza. Liache Neno lake lizame ndani yako kabisa na kukusaidia. Pili, jipe muda wa kutosha kwa ajili ya kujifunza kwa makini ili uelewe vizuri mistari inayohusika na hapo utaweza kuliongoza kundi kwa ufanisi. Kama utafanya haraka unapojifunza Biblia mafunzo hayo yanaweza yakakosa yale Mungu anayokusudia. Ukiwa umejitayarisha vizuri na kwamba ukweli wa Mungu umekushika barabara kuna uwezekano mkubwa zaidi kwamba kundi lako litaipata hali hiyo pia.

Baada ya kusoma mistari husika mara kadhaa, anza kwa kutumia ufupisho ili kuyavunja vunja hayo mawazo yaliyomo. Tafuta mahali aya zinapoanza na kuishia. Jiulize kama hili ni wazo kamili, au limeendelea kwenye aya inayofuata. Wazo ni nini hapa?

Baada ya kufupisha mistari, anza kwa kuweka kwenye chati yote uliyoyaona na yote uliyoyafasiri na matumizi yake. Baada ya kumaliza hilo, uko tayari kutengeneza maswali. Kuuliza maswali ambayo yatavuta wazo kuu kutoka kwenye kila kipengele. Maswali yako yanatakiwa kufuata mtiririko ambao mistari hiyo imeandikwa. Kumbuka, tunayajifunza maandiko hayo kwa utaratibu uliopangiliwa.

# Niongozeje?

Baada ya kuunda maswali kutokana na maandiko, uko tayari kuongoza kundi lako katika mafunzo. Kumbuka: usijibu maswali yako mwenyewe. Kama kundi hawaelewi swali, basi badilisha maneno. Kila mara warudishe kundi kwenye maandiko kupata majibu.

Kumbuka kuyaendea Maandiko kama vile kuendea kitabu, ambacho tunafungua ili kujifunza kutoka humo. Mara nyingi kadiri iwezekanavyo, acha Maandiko yajiongelee yenyewe.

# Kutathimini Uongozi Wako

Baada ya mafunzo ya siku moja, unaweza kutaka kupitia orodha hii wewe mwenyewe, au kumkaribisha Mkristo mwingine katika kundi lako la kujifunza ili muipitie orodha pamoja. Kabla hujaanza kwa nini usimshukuru Mungu kwa majibu mahususi ya sala katika mafunzo uliyoongoza. Kwa vyovyote vile unavyofikiri mafunzo yalikwenda, unaweza kumshukuru kwamba anaweza kutumia Neno lake kwa mafanikio kwa kila mtu aliyehudhuria.

**MATAYARISHO YAKO**

1. Unafikiri ulitumia muda wa kutosha kujitayarisha?
2. Uliweza kupata uelewa mzuri kwenye mafundisho ya msingi? Je uliyaacha mafundisho hayo yakushikilie?
3. Matayarisho yako kwenye sala: Je unataka kufanya mabadiliko katika yale uliyoyaombea unapojitayarisha kwa ajili ya mafunzo yanayofuata?

**MTAZAMO WAKO**

1. Ulimtazamia Mungu kufanya kazi katika hayo mafunzo?
2. Uliweza kuwaonyesha mtu mmoja mmoja wakajua kwamba wanakaribishwa, kwamba mtu mwenye swali au tatizo atake kuongea na wewe?
3. Ulikuwa radhi kujifunza kutoka kwa wengine katika hili kundi?

**MAZINGIRA**

1. Je yalikuwa yasiyo rasmi na ya asili?
2. Kwa ujumla, watu walijisikia huru kuchangia?
3. Ni kwa njia zipi uliweza kuwasaidia watu na kuhamasisha ushiriki wao?

**MUDA**

1. Kama ungekuwa unaongoza mafunzo yaliyoko kwenye aya hii mara nyingine ungebadilisha kasi yake?

2. Uliweza kuanza na kumalizia kwa namna iliyopangwa?

**MAJADILIANO**

1. Orodhesha vitu ulivyojifunza katika kuendesha mjadala kisha tafakari:

   a. Je kundi lako lilielewa mambo muhimu ya mjadala?

   b. Je kundi liliingia kwenye Maandiko kutafuta majibu?

   c. Uliweza kujizuia usijibu maswali yako mwenyewe? (Lakini uliweza kuchangia mara kwa mara, kama mmojawapo katika kundi?)

   d. Je ulibadilisha maneno ya maswali pale ilipohitajika?

   e. Je uliweza kuhamasisha jibu zaidi ya moja kwa maswali mengi?

   f. Kuna kitu chochote ambacho ungependa kumuomba Bwana afanye katika watu ambacho kingesaidia katika kushiriki?

   g. Je kuna mtu fulani ambaye ungeweza kumsaidia katika kushiriki? Ongea naye mwenye.

**MADHUMUNI**

1. Majadiliano yalionyesha mawazo makuu katika hiyo aya? Je haya yalitamkwa ili watu waweze kuyachukua katika fikra na matendo yao?

2. Je, mawazo yaliyokuwa yanaongoza yalifungwa pamoja mwishoni kutoa picha ya jumla?

3. Umeridhaka kwamba mafunzo yalifikia lengo lake – Je baadhi ya watu walionekana kuchukua kweli zilizomo kuzitumia katika maisha yao?

# MAMBO YA KUTAFAKARI KWA UJUMLA

- Tegemea **mistari ya maandiko** ijibu maswali yatakayojitokeza, na siyo huyo kiongozi.
- Jaribu kubakia kwenye aya inayoongelewa. Kuna wakati ambapo maelezo ya ziada yanahitajika kutoka sehemu nyingine za Maandiko, lakini jifunnxze kufanya kazi kwa kutumia ile mistari iliyo mbele yako.
- Baki nani ya mada inayozungumziwa – Ni rahisi kuchepuka na kutoka kwenye mada.
- Ni muhimu kwa kila mtu kuchangia ili kundi liweze kujifunza. Kwa wale ambao wanaoweza kuongea sana wanahitaji kufikiria Yule ambaye ni mkimya na kutoa fursa kwa mtu huyo kuchangia.
- Pale watu wapya wanapojiunga na kundi, inaweza kuwa jambo la msaada kuuangalia tena muongozo.

**P**ale unapouliza maswali, hakikisha unawapa kundi muda wa kutafuta maelezo katika mistari ya maandiko. Kuna wakati itaoneka kipendi kirefu cha ukimya kinapita baada ya swali. Kuwa mwangalifu usiharakishe, kwa sababu watakuwa wanatafuta majibu kwenye mistari.

Maswali mengi yatapata jibu zaidi ya moja, kwa hiyo jisikie huru kusubiri majibu zaidi kutoka kwenye kundi. Baada ya jibu la kwanza, unaweza kuhamasisha maoni zaidi kwa kusema, “Jibu zuri”, au Kuna mtu mwenye kitu kingine cha kusema?

Kumbuka kwamba mjadala wenu utaendelea taratibu mara chache za mwanzo mnazokutana, lakini utakuwa bora zaidi pale kila mtu anapokuwa amezoea. Kwa wengine, yaweza kuwa mara yao kwanza ambapo wamewahi kujadili Biblia kwa njia hii.

Usijali kamam baadhi ya michango itaonekana kwa kiasi Fulani ni ya ajabu au tofauti. Kumbuka, Mungu anafanya kazi na kiongozi hawajabiki kunyoosha mawazo ya kila mtu. Wajibu wako ni kumfanya kila mtu aingie kwenye NENO na kuacha NENO liwanyooshe! Baadhi ya watu wanatabia ya kuibua matatizo. Waombe wakae na maswali yao mpaka baada ya mjadala ambapo wewe unaweza kuongea nao kibinafsi. Hata hivyo, hakikisha umeongea nao baadae.

Wakati mwingine, wakati mjadala unaendelea, mshiriki anaweza bila kutegemewa kuleta jibu la swali ambalo hujauliza bado. Katika hali kama hii, jadili swala hili wakati huo huo linapotokea. Kwa msisitizo, bado unaweza kulitaja hilo swali kwa utaratibu sahihi ulioko kwenye muongozo wako na kukumbushia maoni yaliyotolewa kwenye mjadala juu ya jambo hilo.

Kuna nyakati ambapo mjadala unapamba moto sana, na gafla unagundua kwamba kila mtu ametoka nje ya mada na muda umekwisha. Unataka kuwa na mjadala mzuri, lakini pia unatakiwa kumwacha Mungu aongee kupitia hiyo aya. Kama utafaulu kufanya tu nusu ya aya, kundi laweza kupata tu nusu ya lengo. Jifunze kulirudisha kundi nyuma pale wanapotoka nje ya mada, na kuendelea na swali linalofuata.

Baada ya kila kipindi, imarisha uongozi wako kwa kupitia maswali ya tathmini kwa viongozi ambayo yametolewa kwenye muongozo huu (ukurasa?-?)

Mungu anaweza kufanya kazi katika mafunzo ya Biblia ambayo yanawatu wachache tu ndani yake, au katika kundi kubwa zaidi. Hata hivyo uzoefu unaonesha kwamba pale kundi linapopanuka na kuzidi watu 7 au 8, mjadala hautatoa matunda vizuri hivyo kuna kitu kitapotea. Kama lengo lako ni kuwa na mjadala wa wazi na ukweli katika neno la Mungu, ni vizuri zaidi kudumisha kundi dogo. Kama kundi litapanuka na kufikia ukubwa ambao si mzuri fikiria kuligawa katika makundi mawili madogo na kumfundisha mtu mwingine kuongoza hilo kundi lingine.

Makundi madogo yanaweza kuwa ufunguo wa kweli kwa ukuwaji wa Kanisa, kwa njia zote mbili yaani Kiroho na Kimwili.

# NGUVU YA KUNDI DOGO

Kuelewa nguvu ya kundi ni kitu cha muhimu sana kwa kila kiongozi wa kikundi. Mara nyingi makundi huanza na kukutana kwa msisimko mkubwa, lakini baada ya muda mfupi hushindwa. Ni kwa nini hili hutokea? Kunaweza kuwa na sababu nyingi, kwa mfano kiongozi ambaye hajali hisia za wanakikundi, tofauti za hulka ndani ya kikundi, au kutokuwepo kwa mpango madhubuti.

Kama kundi linashindwa, kila mara kuna sababu. Hata hivyo, kus hindwa hakutatokea kama utakuwa mwangalifu katika kanuni chache za msingi za nguvu za kikundi. Baadhi ya makundi hufanya kazi bila kwanza kufikiria ni kitu gani hufanya kundi liweze kufanya kazi vizuri. Wanadumu kwa sababu wanatenda bila kujua ile misingi ya nguvu za makundi.

**OBJECTIVE VS. SUBJECTIVE**

Makundi hufanya kazi katika hatua mbili za msingi: **objective** and **subjective**. Kama haya mawili hayakusaidiana basi huyo kiongozi wake atakuwa matatani.

Upande wa objective wa kundi unaelezewa kwa jukumu lililopo, yaani, kujisomea Biblia, mkutano wa maombi, mkutano wa bodi, kwaya n.k.

Upande wa subjective unahusika na mahusiano ya ndani ya kundi, pamoja na mtu binafsi kuangusha sehmu ya kundi. Makundi yameundwa na watu wenye hisia zao, ubaguzi, mahitaji na malengo yao binafsi.

Kila mtu katika kikundi atajiuliza kimya kimya, “Mimi nina nafasi gani katika hiki kikund i? Watu watayakubali maoni yangu? Nitafanyaje hili kundi wanione kwamba nina akili sana, mimi ni mwema, ni wa kiroho, au kingine cho chote anachoona kwamba kinakufanya ustahili kuheshimiwa? Utanikubali kama nitakuja kitofauti?” Hadi pale mtu atakapopata majibu kwa maswali haya, atakuwa hajawa tayari kiukweli kuendelea na jukumu hilo. (Kujifunza Biblia, sala, nk.).

Hatua hii ya subjective ndipo matatizo halisi hutokea, na tunahitaji kuiangalia kwa ukaribu sana. Je, umewahi kuona ni jinsi gani baadhi ya makundi hayafanikiwi kutimiza lengo lo lote? Huanza na Isaya 1, lakini huendelea tu hadi mistari miwili ya mwanzo, au wanapanga ibada, lakini nusu saa baadaye wameamua kumkaribisha kiongozi wa ibada. Badala ya kuendelea na jukumu lililo mbele yao, wanakikundi huanza kubishana, kufanya mzaha, kila mtu anaongea wakati huo huo, au hakuna mtu anayeongea kabisa!

Kila kundi lazima lizingatie kwa yote mawili, yaani upande wa objective na subjective. Makundi ambayo yanazingatia kama vipofu kwenye jambo hili wako kwenye hatari kubwa zaidi. Baada ya muda, uhusiano wa kundi yatasababisha mshindwe kulifikia lengo. Ukiwa kama kiongozi, unahitaji kujifunza jinsi ya kushughulikia mivutano na matatizo. Jifunze kutambua matatizo katika kiwango cha subjective. Jaribu kutambua hisia, kwa sababu ni mara chache wanashirikisha kundi hisia zao. Mtu hawezi kusema, "huku kujisomea Biblia kunachusha kweli", badala yake huwa wanaacha kushiriki, wakiketi tu kwenye viti vyao au kuangalia nje dirishani. Watakuwa wanawasiliana kwa njia Fulani badala ya nia ya maneno. Usidanganyike, huyo aliyelala anasema kitu! Hata maneno yanaweza kupingana na hisia zetu. Naweza kuwa nimekasirika, nikiwa na uso umekunjamana lakini nikasisitiza kwamba sijakasirika. Watu wanawasiliana kwa njia nyingi mbali mbali, kwa hiyo tujifunze kutambua maana za mawasiliano ambayo hayatumii maneno.

Pengine njia ya hakika kuliko nyingine ya kujua kinachoendelea katika kundi ni kujiuliza swali: "Ninajisikiaje sasa hivi?" Kama nimekasirishwa, nimefadhaishwa au ninajitetea, basi kuna kitu kisicho sawa. Kama hilo tatizo liko wazi, basi liweke wazi na kulishughulikia. "Naona kama baadhi yenu kuna kitu kimewaudhi. Kuna mtu angependa kuongelea jambo hili?" Mara hisia zilizofichika zikishaongelewa, linaweza kuwa jambo zuri badala ya kuwa jambo baya kwa kundi. Si jambo la ajabu nyakati zenye manufaa makubwa kabisa katika kundi kutokea pale tunapoacha kuzingatia lengo (kujisomea Biblia, nk.) na kuhamishia kwenye subjective.

Mama mmoja kijana alikuwa mshiriki katika kundi dogo la kujisomea Biblia. Alichangia kwa uhuru katika kila mkutano. Siku moja alikja na kuketi kimya kwa nusu ya kipindi hicho. Kiongozi aligundua ukimya huu na alisitisha mafunnzo ili apate kujua ni jambo gani lililokuwa linamsumbua huyo mama. Huyo mama akaanza kutoa machozi na kuwashirikisha jinsi mama yake alivyokuwa anaumwa mahututi. Mara moja kundi liliungana na yule mama katika maombi kwa ajili ya mama yake na kumfariji huyo mwenzao. Hilo kundi lilibadilika kutoka kwenye kundi la kujifunza na kuwa kundi lenye upendo na kuwajali wengine. Kutokana na mazingira kama hayo, ambapo huonekana yanao uharibifu, tunajifunza somo la thamani kubwa kutuhusu sisi wenyewe, mahusiano, magombano, upendo, msamaha na uaminifu. Kwa maneno mengine, tunajifunza kwa uzoefu maana ya maneno ambayo tumeyaongelea mara nyingi kutoka kwenye Maandiko.

## MPANGILIO WA MAHUSIAN

Wanapokuwa katika makundi, watu hufanya mambo kwa njia ambayo tunaitegemea. Baadhi ya njia wanazotenda mambo husaidia na nyingine hukwaza. Hapa kuna aina hizo:

- Kuongea kupita kiasi – kila wakati anakuwa na kitu cha kusema kuhusu kila kitu
- Mtu mwenye haya – mara chache sana atasema kitu chochote

Mwangaliaji – huangalia kila kitu, lakini yeye hatendi

Mchekeshaji – kila mara anacho kitu cha kuchekesha

Myumbishaji – Mwenye ufahamu mwingi ambaye hutoa michango isiyohusika

Mbishi – ana maoni yenye nguvu na hakubali hoja zake kushindwa kirahisi

Mwenye ajenda ya siri – ana kitu kingine akilini, lakini hapendi kukionyesha

**KUSHUGHULIKA NA HIZI AINA TOFAUTI**

*Anayeongea kupita kiasi*
Mchukue mtu huyu na kuongea naye wewe binafsi bila kumshambulia au kumuumbua. “Paulo, nahitaji msaada wako katika kuwafanya waongee zaidi. Ninashukuru sana kwa mawazo unayotoa, lakini nisaidie kuwafanya wengine katika kundi nao wachangie. Pale ninapouliza swali, naomba usiwe wa kwanza kujibu. Hebu tuwahamasishe na wengine kujiunga na kutoa mawazo yao.”

*Mwenye Aibu*
Huku ukitumia majina yao ya kwanza, mwulize mtu swali moja kwa moja. Hili litaanza kuwafanya wachangie zaidi. Sema vitu vizuri kuhusiana na jibu lake, kwa mfano: “huo ni mtazamo mzuri”, au “umejibu vizuri!”

*Mtazamaji*
Jaribu kumvuta mtu huyu ndani kwa kutumia swali la moja kwa moja. Wakati mwingine watu huwa watazamaji kwa sababu hawana hakika kama kundi litawakubali. Kwa hiyo, wavute ndani kwa upole na kuwakubali.

*Mchekeshaji*
Mtu huyu anaweza kuwa wa msaada mkubwa kwa kundi kupunguza msongo wa mawazo na kwafanya watu wakae kwa starehe zaidi. Hata hivyo, kuna wakati mwingine kichekesho kinatolewa wakati mbaya. Kama hili linakuwa tatizo, mchukue pembeni mhusika na kumwambia kuwa unashukuru kwa kipawa chake cha kuchekesha. Lakini, msaidie aone kwamba wanatakiwa kutumia hekima wanapochekesha.

*Mpotoshaji*

Aina hii ya mtu inaweza kuwa tatizo kubwa kwa kundi kama hatashughulikiwa kwa ufundi mkubwa. Jifunze kumrudisha mtu huyu kwenye mada na maandiko yanayohusika. Unaweza kutoa kauli kama, “Hiyo ni mada nzuri. Labda tunaweza kuiongelea zaidi wakati mwingine.” Bila kumpa mtu huyo muda wa kujibu, liongoze kundi lirudi kwenye topiki husika kwa kutumia swali jingine.

*Mbishani*

Kama mtu anaendelea kuwa na matatizo, mchukue pembeni na kuongea naye. Heshimu mawazo yake, lakini sisitiza umuhimu wa kuwaacha wengine katika kundi kutoa maoni tofauti bila kujisikia ulazima wa kutoa changamoto kwa mawazo mengine kwa njia ya mabishano. Kama kiongozi ataruhusu aina hii ya mtu aendelee, kundi litaacha kuchangia kwa kuogopa kubishiwa. Kama mtu huyu akianza ubishi, ni muhimu kwamba kiongozi anadhibiti hali. Tambua thamani ya mawazo yote mawili, na kusema kwamba wengine pia wana maoni yenye nguvu kwenye masuala haya. Waambie waache ubishi wao na kuendelea na kujifunza.

*Ajenda iliyofichika*

Kama utahisi kwamba kuna mtu anakwaza mafunzo basi ni muhimu kulishughulikia chochote kinachomsumbua mtu huyo. Kabla hujachukua hatua yo yote mwombee kimya kimya. Wakati mwingine hili ndilo jambo pekee linalohitajika kufanyika. Hata hivyo, kama utaona kuna umuhimu wa kufanya hivyo, unaweza kumsaidia mtu huyo wakati wa mafunzo na swali na kauli vyaweza kusaidia, kwa mfano: “June, leo uko kimya sana. Kuna tatizo?” au “ Inaonekana uko mbali sana leo, kuna kitu tunachoweza kukiombea pamoja na wewe?”

## MAZINGIRA YA KUNDI

Mazingira ya kundi lolote ni kitu muhimu sana. Kama watu wanajisikia joto, upendo, kukubalika, kundi hilo litakuwa na afya. Kukiweko na mazingira sahihi, kundi litaweza kuepuka matatizo makubwa au tabia haribifu.

Kila mtu katika kundi anatakiwa kujisikia anakubaliwa na kusiweko na hali ya kuhukumiana kabla hawajawa huru kushiriki. Mara nyingi matatizo huingia pale mtu Fulani anapojifikiri “amefika” kiroho, au ana utambuzi maalumu katika mapenzi ya Mungu ambayo ni wengine wachache tu wanao kama yeye. Pale hili linapotokea, hatuwezi kujizuia kuwahukumu wengine. Pale tunapoanza kujiona wenyewe kama tulivyo hasa (wenye dhambi, walioanguka ambao hata hivyo tunapendwa na Mungu), basi, sit u kwamba tuanaweza kuacha hali zetu za asili za kuhukumu, bali pia tunaweza kuwa wakweli.

Ni furaha kubwa kuwepo katika kongamano hili. Nataka kuwashirikisha kutoka katika uzoefu wangu wa kuwa mchungaji ,ambapo naamini ni umuhimu wa masomo ya Biblia pamoja na mahubiri niliyofanya kanisani,hili sio somo kamili japokuwa ninao ujumbe, ni ujumbe mzuri na nitauhifadhi mpaka mwisho. Ninachotaka kufanya ni kutoa mahubiri ya kina, nataka kuanza kujielezea mwenyewe, hasa kuelezea juu ya safari yangu mwenyewe, nafikiri ni muhimu kwenu kufahamu jinsi nilivyoweka vipaumbele katika utoaji huduma ya kiroho hasa ninayoifanya hivi sasa katika kanisa la Kiprebysterian la Berkeley na huduma niliyofanya katika kanisa la Union kule Manilla na kabla ya hapo katika kanisa la chuo cha Kipresbyterian lilipo kule Seattle na ndipo unapoweza kujua sio tu katika mtazamo wa kithiolojia, lakini katika thiolojia yangu mwenyewe, ambayo ni muhimu sana katika huduma binafsi.Mimi ni kizazi cha tatu cha Wakalifornia na nilikulia karibu na mlima Shasta. Familia yangu ilikuwa ni nzuri, yenye uhuru, yenye furaha, yenye hamasa, lakini siyo ya dini,niliacha kuhudhuria kanisani miaka ya mwisho ya masomo yangu ya elimu ya juu ya sekondari, na niliendelea kutohudhuria miaka miwili ya kwanza katika chuo cha Kalifornia huko Berkeley, haikuwa sehemu ya maisha yangu kabisa, katika mwaka wangu wa pili wa chuo nilikaa katika bwalo la Barrington, ambayo ilikuwa na mpaka sasa si sehemu nzuri, tulikuwa na heshima yakuwa bweni pekee Marekani lililopo kwene orodha ya kamati ya shughuri zisizo za Kimarekani. Zaidi ya watu 250 waliishi katika bweni hili la Barrington kipindi hicho, hatimaye nikawa raisi wa bwalo hilo, siku moja nikiendesha gari huko Barrington, bado ipo pale. Kukupeni ninnyi raha kidogo illiyokuwepo, kulikuwa na michoro kila sehemu, kwa sasa kwa sababu kuna migomo ambayo inaendelea huko Berkeley. Mchoro mmoja ambao nilidhani ni alama ya bwalo la Barrington ilikuwa juu ya mlango wa ,mbele, yakiwa - sijawahi kumsikia, nilikaa miaka yameandikwa kwa maandishi makubwa meusi yenye herufi zilizopuliziwa “Ondoka hapa”Katikati ya mwaka wangu wa pili nilialikwa na rafiki yangu kwenda katika kujifunza Biblia katika kikundi. Kundi hili dogo lilikuwa likikutana mara moja kwa wiki katika chumba na walikuwa wakijifunza kitabu kutoka katika agano jipya: Ilikuwa rahisi hivyo, Walikutana kwa muda kama wa saa moja kuchangia mawazo ya aina mbalimbali kuhusiana na Agano jipya, Naikumbuka picha ya kwanza niliyoipata nilipohudhuria katika kikundi cha kujifunza Bibilia, nilifadhaika kuona watu wa umri wangu, vijana wa rika kubwa, wakisoma Agano jipya kwa macho ya kiutu uzima na wakiiongelea kwa makini pasipo mzaha. Ulikuwa ni uzoefu wa mzuri ajabu. Sikuwa na Bibilia kwa kipindi hicho kwa hiyo ilibidi nisome na mtu mwingine. Nilifurahi sana kiasi nikasema nataka kuendelea kuja kujifunza Biblia. Tulikuwa na Bibilia nyumbani lakini, sikuwa nayo kule Berkeley, Bila kujua tafsiri za aina mbalimbali niliishia kununua Biblia isiyo sahihi, Ile ya King James. Wiki iliyofuata nilipoenda katika kikundi kujifunza Bibilia waliniambia hiyo Biblia hiyo hatuitumii, tunatumia RSV” Ilibidi niende nikanunue Biblia nyingine, nilikuwa hivyo, sijawa hata mkristo kamili bado, lakini nimeshanunua Biblia mbili katika wiki moja. Nilinunua Biblia aina ya RSV na nikaanza kuhudhuria mara kwa mara katika kundi hilo dogo.

Nilianza kuhudhuria kundi la kujisomea Bibilia lilopo chuo katika kanisa la kwanza la Kipresbyterian lilipo Barkeley hicho kilikuwa kipindi cha mvua, wakati wa masika nilienda katika kongamano katika Ziwa Tahoe, wahubiri wawili walikuwepo, Edward John Camell kutoka seminari hii, na Rovert Boyd Munger , nitakumbuka badiliko kubwa katika maisha yangu kilichotokea siku hiyo ya kongamano, Bob Munger alielezea juu ya kitu. Alisema “Unapokubali juu ya imani na thamani ya Yesu Kristo na ukawa tayari kuamnini uaminifu huo, hapo ndipo upo tayari kuwa Mkristo” alisema hayo mbele ya kundi zima, sio kwangu mimi pekee lakini vile alivyosema alikuwa kaniambia mimi moja kwa moja, nakumbuka nilipoenda ziwani nakusema nimeamua kuamini uaminifu huo wa Yesu Kristo.Haya yalitokea nikiwa bado mdogo, niliporudi Berkeley nilikua haraka sana, na nilijihusisha sana na mafunzo ya Biblia katika makundi na kama nilivyoelezea baadaye nikachaguliwa kuwa Rais wa Bwalo, vile vile Rais wa kundi la chuo katika kanisa la kwanza la Kipresbyteria.Wakati huo vile vile nilikuwa naendelea kuwa mshiriki mahiri katika kundi hili dogo la kujifunza Biblia. Tuliona vitu vya kustaajabisha katika mwaka wa mwisho wa chuo. Tuliona watu katika bweni lile wakibadilika na kuwa wakristo karibu kila wiki mwishoni, ilitokea tu, katika njia moja ama nyingine, walikua wakitoka gizani/porini, na Mungu aliibariki huduma ile. Katikati ya mwaka wangu wa mwisho japo nilikuwa nabobea katika sheria/ Siasa na sayansi ya jamii, niliguswa na kile kilichokuwa kikiendelea kwenye mafunzo ya Biblia katika kikundi na kwa kuwa nilipata nafasi ya kushuhudia kama mkristo nilimwambia mchungaji, Bob Munger, “Unajua hiki ndicho kilichonibadilisa mimi. Natamani kama ningekuwa mtumishi “ Akajibu, Kwanini usiombe nafasi seminari ya Princeton?” Na niliomba nafasi katika seminari ya Princeton, naamini nilikuwa kijana mzuri, rasimali, mtu safi ambaye hawajawahi kumwandikisha. Kanisa la kwanza la Berkeley walinipangia

**"Nikiweza kuwafanya watu wakatafakari ujumbe kwa kina, hiyo italeta ushawishi yenyewe."**

kukutana na Lynn Bolik mkereketwa na mfuasi mkubwa wa kiprotestanti, alinisaidia sana nilipokuwa mwaka kwanza huko Princeton, wengine waliohofu kwamba nitapotea kabisa kwenye mrengo wa kuamini juu ya uhuru wa mtu(mfumo huria),walihakikisha kwamba naenda kwenye kongamano la Navigator lililofanyika Star Lanch kabla ya kwenda Princeton, nilipoenda Princeton, nilipata uzoefu wa kuelewa mambo mengi ya zamani, nillifanya uvumbuzi mwingi wa mambo yote ya kithiolojia yaliyokuwa ni muhimu kwangu kithiolojia: niligundua juu ya John Mackay, mhubiri mkubwa ambayemizuri mitatu Princeton na baada hapo nikaanza kutoa huduma ya kichungaji, ila kitu kilichonitokea kwanza nilipokuwa katika bwalo la Barringtonkule Barkeley kiliacha alama kubwa isiyoweza kufutika. Kule Princeton kipindi hicho tulihitajika wote kwenda kuinjilisha katika makundi , kitu ambacho sikukipenda, haikuwa dhamira yangu kwenda makanisani na kusema maandiko matakatifu wakati wa ibada na kuongea na vijana na baada hapo kwena kwenye chakula cha mchana na familia. Tulikuwa tukiiwakilisha seminari na tulikuwa tukifanya vizuri, hasa has asana ay kidogo. Nilifanya hivyo zaidi ya mara manne mpaka nilipofikiria kuachana na huo mpango, karibu na mara ya mwisho niliendа Jenkintown nje ya Philadephia, nilipata chakula cha mchana na familia ya Kelly, kulikuwa na kijana katika familia hiyo aitwaye Glen,aliyekuwa ndiyo ameanza kusoma katika chuo cha Princeton kipindi hicho alikuwa nyumbani. Kuzungumzia maswala yahusuyo Mungu- hakika naamini sana juu ya haya. Nikasema "Ooh unatokea chuo cha Princeton. Natokea seminari ya Princeton. Inapendeza sana, inabidi twende wote mpaka chuo" Akasema "Safi" Kwahiyo wiki ijayo tutaenda wote na nikamwambia "Unajua Glen, nilipokuwa Berkeley nilijihusisha na masomo ya Bibilia katika kikundi na ilimaanisha mengi kwangu. Sijawahi kufanya hivyo hapa Princeton. Mnafikiria jamani mnaweza kupenda kuwa na kundi la kujifunzia Bibilia? Akasema, ngoja niwaulize rafiki zangu tunaokaaa chumba kimoja, ili kuanzisha kundi dogo la kujifunzia Biblia hapa Princeton. Nilijihusisha karibu na makundi saba kwa mara moja kwa sababu kila kundi lilitaka nilisaidie, hiyo ilikuwa huduma yangu kwa miaka yote mitatu hapo Princeton. Makundi yalikutana saa 10 jioni, saa 12 asubuhi au saa 10:30 jioni , siku zote walitumia saa nzima na nilitumia kanuni ile ile kama ya Berkeley, majadiliano rahisi yenye dhima tofauti tofauti katika vitabu tofauti vya agano jipya. Baadhi ya wiki Mtume Paulo alishinda na zingine alishindwa, lakini sikufadhaishwa na hilo. Nilijaribu kuangalia ujumbe huo katika Biblia na wanafunzi wenzangu na kujua nini kimo ndani ya ujumbe huo,nilichogundua kilikuwa sawa na nilichokigundua kule Barrington, kama ningepewa muda, mtu mmoja kuangalia ujumbe, so muda mrefu wangevutiwa nao, Upembuzi yakinifu wa kujifunza Bibilia katika makundi ndivyo nilivyoita. Silipendi neno "makundi ya uinjilisti ya kujifunza Biblia " Mara nilipoongea na viongozi kutoka vyuo mbalimbali, niliwaambia msiite Makundi yenu ya kujifunzia Biblia, Makundi ya uinjilisti ya kujifunzia Biblia , tuyaite, Makundi ya kujifunzia Biblia kwa kina, Kwanini tulipe kitambulisho cha kipekee? Ngoja tusome ujumbe maana inafaa na kama Mungu afanye uinjilishaji kama akichagua hili. Hivi sasa California ya kaskazini vyuo mbali mbali vinaita masomo ya Biblia katika vikundi, Makundi ya kujifunzia Biblia kwa kina,Niliwaona vijana kadhaa kule Princeton wakibadilika na kuwa wakristo katka makundi hayo ya kujifunzia Biblia, sijawahi fanya chochote cha kuwalazimisha wawe wakristo ama kuwashurutisha, ilitokea tu, uvumbuzi huu wote uliijenga sana huduma yangu ya utumishi na staili ya uendeshaji kimsingi kabisa vile vile na njia zangu za kithiolojia,Kwa uhakika kabisa naweza kusema huduma zangu za kidini kule Seatle, Manila,na Berkeley zilitokana na msingi huu: kama ningepata watu wakafikiria kiumakini ujumbe huu ingewavutia kwa namna moja.Kanuni hiyo iliniondolea msukumo, wala sikutaka kutumia akili sana au kuwa na mpango madhubuti. Niliyohitaji kuyafanya ilikuwa nikuwafanya watu watafakari ujumbe japo mara nyingine inahitaji stadi Fulani kuwanya watu wafanye hivyo. Niliamini thiolojia nzuri ni ile ambayo inaanza na ujumbe. Sio kuchukua maswali yote ya dunia nzima alafu unaanza kuyatafuta majibu katka Biblia ili uiambie dunia, ila ni kupata maadili na msimamo kutoka katika ujumbe na kutumia ujumbe huo kuijibu dunia, katika kitabu kilichoandikwa na Thielecke volume 2, **Theological Ethics,** alielezea utofauti wa Thiolojia kati ya Paulo Tillich na Karl Barth, na alitumia mbinu hii kutofautisha njia hizo mbili za Kithiolojia. Alionyesha kwamba Paul Tillich ambaye alihusika sana na uhusiano, alianza na namna mbali mbali jinsi dunia ilivyo, na ndio maana thiolojia yake imesimamia kwenye uwepo na ubashiri/kuhisi. Alianza na mambo mbali mbali yaliyomo duniani, aliuliza maswali kuhusu uwepo na kuangalia mtazamo wa kithiolojia, Thielecke alionyesha hayo kwa utofauti, Karl Barth alianza na ujumbe na akaiangalia dunia na wapi mgongano huo umetokea. Aliutumia huo kama mfano wake wa mbinu ya kithiolojia katika kitabu kinachoitwa Barmen Declaration of 1934, kilichoandikwa na Karl Barth, Martin Niemoller na Wilheim Niemoller. Inavutia kuona kwamba makala zote saba katka Barmen Declaration zimeanza na ujumbe na kutoka kwenye ujumbe inaenda moja kwa moja kuona dunia ilivyo, kwa mfano Makala no. 1 inaanza na Yohana 14. Mimi ndimi njia,

**"Mimi nilishawishika kuamini kwamba mahubiri yenye nguvu/ufanisi mkubwa kuliko yote, ni yale, yenye kuvutana kurefu, yenye ufafanuzi wa Kibiblia."**

ya kweli na uzima hakuna ajaye kwa Baba ila kupitia kwangu". Ndipo inakuja makala: Yesu Kristo ni neno moja tulipasalo kulitii, katika maisha na kifo, kinyume cha hapo: tunakataa mafundisho ya uongo kwamba kuna maneno yaliyo na mamlaka sawa ambayo inabidi tuyasikie mbali na hili neno moja tu la Yesu Kristo" kujua kwamba Barth alianza na ujumbe, na akaupeleka mpaka kwenye UNAZI – Ujerumani mwaka 1934, na aliiona migongano. Hakuanza kuelezea juu ya uwepo wa mwanadamu na kifo na baada hapo kuhisi juu ya uhusiano uliopo, katika maneno mengine, alianza kama mtu wa mafundisho ya Kibibilia, Barth kama mwanateolojia alisafiri safari ya aina moja: alianza na maelezo kuhusu Roma, maelezo kuhusu Uroma, na ndipo alipoendelea na mafunzo maalumu ya Thiolojia. Kithiolojia na kimaadili/miiko na uzoefu nilikubali kabisa juu ya kusoma Biblia katika makundi na baada ya hapo thiolojia yangu binafsi, niliuchukua mtazamo huu wa Kibbilia/Kithiolojia ndio maana nafikiri bora nikawa mwanathiolojia wa Kibiblia ninayefuatilia na kujua vitu vingi kuhusu Bibilia kuliko kuwa mwanathiolojia wa kufuata kanuni na taratibu tu. Nilishawishika kwamba uinjilisti wa kweli utatoka njia rahisi isiyo tata ipatikanayo kwenye uchambuzi yakinifu wa masomo ya Biblia,pale ambapo unakuwa huelewi kwamba unainjilisha. Falsafa yangu nzima ya uinjilishaji ni hatua zaidi ya elfu moja kila moja pekee ambazo zilitokea kutokana na urafiki,katika mazingira ya kawaida kabisa, watu walio wengi wa Berkeley waliompokea Kristo wanatokana na makundi ya kujifunzia Biblia, Makundi yanayojifunza Biblia kwa kina, Vikundi vya maombi, uhusiano ambao watu wanapata nafasi ya kuona jinsi wakristo wanavyofikiri na kupendana, kuwaona wakristo katika maisha yao ya kila siku.Hukerwa na udadisi wao, baadaye huchunguza na kuwa Wakristo.Mwishoni nilishawishika kwamba mahubiri ya maana na mafundisho ya jitihada ni yale yanayotokana na uchambuzi wa Bibilia, nafikiri niliwaeleza maana ya uchambuzi wa Bibilia, nimeirekabisha maana hiyo na kuwa nzuri toka nilivyoandika kwa mara ya kwanza ambayo ilikuwa katika makala ya Fullers, **Theology, News and Notes**. Hiyo ndiyo ilikuwa makala yangu ya kwanza kuchapishwa kuhusiana na fikra zangu juu ya hili somo. Katika makala hiyo nilitoa maana ya: Mahubiri ya Kibiblia, kimsingi ni mahubiri haya ya Bibilia, kama nionavyo kwamba ni jukumu la kufanya ujumbe ama kutoka agano la kale ama agano jipya kwa pamoja kushuhudia na kueleza Injilia ya Yesu Kristo, na kuufanya ujumbe huu kuwa unaoshawishi na wa haraka katika lugha ya leo. Katika mahubiri kuna upande wa kithiolojia vile vile, kuhubiri si kusema tu kilichoandikwa ni nini, lazima useme ujumbe huu unamaanisha nini. Nionavyo hii inachukua safari nzima ya Mchungaji ama Mwalimu kuufahamu ujumbe na mpaka kwenye utume/ uinjilishaji, hayo ndo mahubiri ya Kibiblia, na naamini hicho ndicho kanisa linalokihitaji, naamini ni njia inayoshawishi zaidi, ya kiinjilisti, na inayofuata taratibu. Ninafikiria sana juu ya mahubiri yanayofuata kanuni na taratibu, lakini naamini kabisa mahubiri sahihi yanayofuata taratibu na kanuni ni yale yanayotokana na kile kilichoandikwa. Nitahitimisha nikiwa nakubali lakini kwa sasa napinga kwanza. Ngoja nifikiri kile kinachoitwa mgongano wa kimahubiri katika mahubiri ya siku hizi na mafundisho katika makanisa ya leo. Siongelei juu ya mgogoro wa uhuru wa kithiolojia au yale yenye mtazamo usiobadilika, huu ni mgogoro wa kanisa zima, ni mgogoro wa kimahubiri, na hii nafikiri ndio sababu kamati ya uchambuzi wa Bibilia imeundwa.Nafikiri kuna aina mbili za migogoro. Mgogoro wa kwanza ambao naenda kuuelezea ni mgogoro wa kimaada katika mahubiri. Nafikiri mahubiri mengi hivi sasa kanisani ni ya mada, ninachomaanisha ni kwamba chanzo cha migogoro inatokana na mada kubwa za imani zetu ambazo huelezewa na walimu kwa wasikilizaji wao, lakini wasikilizaji, husikia kilichosemwa na mtu mwenye mamlaka, na mwalimu au muhubiri ambaye anasema hiki ndicho tunachokiamini, hawaangalii kwamba inatoka kwa nani, wala hawagundui hilo wao wenyewe. Wao huambiwa tu, na hii ndo maana ya uhubiri wa mada wa kimamlaka, Mchungaji kasema, "Mungu anawapenda". Hawalitafuti hilo katika maandiko, wanaambiwa tu.

Najitahidi kuwa muungwana na mahubiri ya sasa yenye mkanganyiko kama nionavyo, lakini ujumbe wa injili unaohubiriwa na wachungaji wengi hutokana na vyanzo vikuu vitatu :-

(1) Ni kuhusu walimu na wahubiri. Kwa maneno mengine, mzigo wa Bwana ambao wachungaji wanao ni chanzo cha ujumbe:hiki ndicho ninachokifikiria kutokana na kutembea na Bwana/kuwa na Bwana.

(2) Chanzo cha pili cha mahubiri inatokana na uzoefu wa mchungaji, nina mashaka kidogo kuhusu ujio huu wa seminari za Kimarekani wa kuhubiri kwa kusimulia kama stori, ambapo utaelezea hadithi yako na inatakiwa impe ujumbe wa kiinjili mtu mwingine. Hii inamaanisha uzoefu wa mchungaji kuwa na Yesu kwa wiki moja ndio kimekuwa chanzo cha ujumbe, Jinsi ulivyo msimuliaji mzuri wa stori ndivyo utakavyoulizwa

ujielezee zaidi kuhusu wewe mwenyewe, kumbuka ule mstari kwenye **Mass Appeal**? Pale ambapo Padre Tim anamwambia Mark, mseminari mdogo aliyekuwa havutiwi kabisa na mahubiri ya Padre Tim. “Hujayapenda kabisa mahubiri yangu, sivyo?” na Mark akasema ndiyo sijayapenda” Padre Tim akasema, “ hujui kwamba watu wameniuliza sana kuhusu mimi mwenyewe mara nilipomaliza kuhubiri!” Padre Tim ni bingwa wa kusimulia stori , ujumbe wake hutokana na matembezi yake ya wiki.

(3) Chanzo cha tatu, ambacho nadhani ni hatari kuliko zingine zote, ni ule uelewa wa ujumla kuhusu kweli Fulani wa wakristo wote, lakini hakuna hata mmoja anayeweza kugundua, Wote tunajua kweli hasa, na hivyo ndivyo jinsi vitu vinavyoharibiwa katika dini zisizo na mpangilio, mkristo mdogo hawezi kujua yanapatikana wapi. Narudia, chanzo cha ujumbe ni vitu vitatu katika mamlaka ya kimahubiri, kwanza ni mzigo wa mchungaji, na nashukuru Mungu maana mara nyingi mzigo huu huletwa na Roho Mtakatifu, sina wasi wasi na hilo. Cha pili ni uzoefu wa mchungaji, na tatu ni kile ninachokiita uelewa wa kweli wa jumla wa wakristo, ambapo kila mmoja anatakiwa kujua. Yote haya yanapelekea kupotea kidogo kutoka kwenye injili,”nje ya injili” “ndani ya ijili” , na maafa makubwa ya kiinjili yakatokea. Mashaka makubwa ya Lutha yalikuwa juu ya injili “extra nos” injili nje yetu sisi: kwa uadilifu wake, inaweza ikasomwa na kupimwa, ni imani ya kihistoria. Mungu aliongea na aweza kueleweka, lakini inapopotoshwa kutokana na uzoefu wangu Injili inakuwa haina msaada. Ngoja niwapeni mfano wa hili, Miaka kadhaa hapo nyuma mimi na familia yangu tulikuwa safarini, tulishindwa kwenda kanisani, tulimsikiliza mchungaji aliyekuwa akihubiri katika radio, alisema anaenda kuhubiri juu ya thiolojia ya matumaini, akisoma maandiko hayo kutoka Warumi 8, hii ilinifurahisha sana kwa sababu huwa nakipenda sana kitabu hicho hasa Warumi sura ya 8. Sura nzima aliyoisoma ilihusu juu ya siri ya uumbaji, kwa maana nyingine iliwekwa katika mipaka ya kutojulikana sio kwa mamlaka yake yeye bali Mungu mwenyewe, Ungependa maandiko yaandikwe hivi aliyaweka hayo kama siri ‘Katika hukumu” lakini Paulo anawashangaza wasomaji wake, aliyeweka hayo kama siri kwasababu ya “Matumaini” hapo ndipo neno matumaini linapoonekana, Mchungaji huyu aliyasoma maandiko haya katika mwanzo kabisa wa mahubiri, na bila kuficha naweza kusema yalikuwa ni mahubiri yenye nguvu na kuvutia ambayo sijawahi yasikia, yalikuwa ni mahubiri yanayoeleweka na niliganda kwenye radio kutoka mwanzo wa mahubiri, mchungaji alihubiri juu ya matumaini, kilichochukua nafasi ni mfululizo wa historia/mikasa ya maisha yake, alisimulia matukio mbali mbali katika maisha na yale ambayo kayaona. Moja kati ya hayo matukio lilikuwa ni kusikitisha, lilinifanya mimi nitoe machozi, ni mtu wa hisia sana, matukio mengine yalichangiwa na baadaye mahubiri yakafungwa kwa maombi. Sikutaka kusema mengi, lakini nilifadhaika sana, katika mahubiri yote hata mara moja hakuacha maandiko yaseme chochote, bila shaka yoyote maandiko hayakuleta mwanga wowote katika mahubiri, mahubiri yalikuwa historia yake mwenyewe ya maisha iliyomfanya ajifunze juu ya matumaini katika maisha. Binti yangu Anne aliniuliza, Baba unayafikiria vipi yale mahubiri?’ nilitaka kusema kitu ambacho ni kizuri kwa sababu, kwa vyovyote, sisi waumini lazima tushikamane. “Vizuri, ngoja nikwambie kitu Anne, Nilitokwa na machozi kwasababu ya baadhi ya maelezo, na huo ndio uliokuwa ukweli, lakini hilo halikumridhisha mwanangu, aliyesema “Unajua Baba, sikuyapenda mahubiri yale?” Majibu yake nilipouliza kwanini wakati mimi nilidhani sio kitu cha kusahau, “ Kuna shida gani na mahubiri yale. Niliona kama, mchungaji ndiye alikuwa akisema, kwamba tuwe na matumaini kwasababu na yeye ana matumaini.” Na huo ndio ulio kuwa ujumbe wake, haikuwa injili, mwanangu amekuwa anajifunza Biblia katika sehemu nyingi, amekuwa akisoma Paul Byer kwa muda wa miaka miwili akijifunza maandiko ya Marko, vile vile na maandiko ya Habakuki.Kwahiyo Anne hakuwa tayari kabisa kuelewa hayo, kwa sababu amezoea kuona injili inatoka ndani ya maandiko, vile vile alikata tamaa kwa sababu maandiko hayakupata nafasi ya kusema. Hapa kuna maandiko mengi yanayo ongelea juu ya matumaini katika maandiko yote ya Paulo lakini hata mara moja Paulo hajaruhusiwa kusema chochote. Badala yake kumekuwa na mlolongo wa masimulizi mengi ya stori, mniamini kabisa lazima maelezo kuhusu yeye binafsi yangeulizwa siku ile, kwasababu hakufanya chochote kizuri, ule ulikuwa ni usimulizi tu wa stori zaidi. Hatari ya mahubiri yale sio hatari ya orthodoxy, kwa sababu yalikuwa ni mahubiri ya kiorthodoxy. Hakuwa na kitu hata kimoja kithiolojia ambacho ningekataa, hata hivyo kwani hiyo ilikuwa ndo jaribio kubwa? Hatari ya mahubiri yale ni kwamba kila mtu aliyesikia mahubiri yale hakupata nafasi ya kuona ni namna gani mahubiri yale yanatokana na maandiko katika injili, waliyasikia tu kutokana na uzoefu wa Mchungaji. Ngoja niwaulize swali kubwa, Kama una uzoefu wa wiki moja, labda uzoefu na Roho Mtakatifu, labda umeota ndoto au maono, waweza kuhubiri hayo siku ya Jumapili?

**“Injili na matukio yako ni mawili tofauti. Kazi ya kuhubiri ni kusisitiza mkazo ambao utakumbukwa na kutendeka.”**

Hapana, kama ni mtu uliyeachana na desturi za zamani huwezi fanya hivyo. Kwa uzoefu wako unakuwa mtu mahiri, lakini inatakiwa uhubiri injili, kwa sababu uzoefu wako na injili ni vitu viwili tofauti. Uzoefu wako waweza tosheleza kutoa ushahidi juu ya injili , na kama mhubiri ni vizuri ukawa nao ili uweze kuonyesha uhusiano au muungano uliopo kati yetu sisi na watu, na hii ndio sababu halisi ya maelezo, na simulizi mbalimbali kuhusiana na maisha yako. Lakini hayo peke yake sio ujumbe, hiyo siyo kiunganishi kati ya watu na maandiko matakatifu. Kiuhalisia, huwatenga kabisa watu na maandiko matakatifu. Inakuwaje katika muda ambao unakosa kabisa matumaini, ama pale ambapo hujali? Uzoefu, mifano, simulizi, kutokana na maisha ya mtu mwingine havitoshi. Asante Mungu kwa ajili ya mama Theresa, lakini yeye sio injili. Matendo yake mema yaliyodhihirika kule Calcuta sio habari njema, ni ushuhuda mzuri wa habari njema, lakini habari njema ni Yesu Kristo mwenyewe. Injili ipo “nje yetu sisi’ Injili ipo ndani ya maandiko, na ni kitu kizuri namna gani pale mtu anapogundua thiolojia ya matumaini kutoka kwenye maandiko. Ngoja nitoe mfano mwingine kuhusiana na tatizo hili, kuna wachungaji wengi ambao hawawezi kuhubiri ibada bila kutoa msemo Fulani usio na ukweli wa imani ya wakristo, hii hutokea kwa sababu wanafikiri inabidi wawafanye watu kufikia maamuzi. Kwa hiyo mchungaji atatoa mahubiri mazuri kutoka katika maandiko, akiyapa maandiko nafasi ya kuzungumza, baada ya hapo hupata kama dakika tano za mwisho za mahubiri kinachofuata kinakuwa ni misemo na nahau mbalimbali ambazo mwenyewe hazielewi na hata wasikilizaji wenyewe hayawaingii akilini mwao. Kwa muda huo watu huweka makaratasi yao chini wanajua wao na mahubiri ndio wanafikia mwisho.

Ukishamaliza kusema kile kilichopo kwenye maandiko usimame. Kama vile nilivyokwisha kusema, nafikiri tatizo kubwa la mahubiri ya sasa ni kuhubiri mada kimamlaka. Sasa hatari yake kinyume chake ni ni kile ninachokiita uhubiri ambao sio wa kitume, pale ambapo matokeo ya utafiti yanaangaliwa kwa pamoja, lakini bila haraka na bila kuwa na subira, bila kufahamu mzigo wa Bwana. Mtu mara nyingine huhalalisha matatizo haya, “ Ndiyo, nashukuru nimewaambia wao ukweli. Nimewahubiria injili” Lakini lazima mkumbuke kwamba katika stadi za kuhubiri na mahubiri sio kwamba kwa sababu umeeleza kuhusu pointi haimaanishi kwamba umeeleweka. Kazi ya kuhubiri ni kuhubiri pointi na kuifanya pointi hiyo ikae vichwani mwa watu na ieleweke. Hiyo ni kutokana na juhudi na maarifa/ ujuzi. Mwishowe hufanya maajabu ya Roho Mtakatifu kuifanya injili hiyo ya kweli na maandiko.

Njia nzuri ya kufanya pointi ieleweke ni kuacha watu waigundue ama waitafute wao wenyewe, jukumu la mahubiri ya wazi ni kumsaidia mtu aone, “ Aaah kumbe ndivyo maandiko yanavyosema. Nimeoona yalipo, Nimeyapata….Nimeayaona.” Kwa manenno mengine, mahubiri ya ufafanunuzi ni kufanya maandiko yaliyo katika agano jipya na la kale yatengeneze pointi au wazo linaloeleweka. Iwe katika kujifunza Biblia katika kundi au kuhubiri kwa ufafanuzi, nafikiri kabisa kwamba hayo ndio mahubiri ambayo kanisa linayahitaji. Ninakubali si kila mara hayo ndio mahubiri ambayo kanisa linayataka bali hayo ni mahubiri ambayo kanisa linayahitaji. Nakubali kabisa kwamba ninyi kama wachungaji lazima mjuhusishe na kusoma Biblia katika makundi ya kujifunzia Biblia. Niliwaambia wanafunzi wangu leo “ Sheria ya kwanza; ili uwe muwasilianaji mzuri lazima uiepuke kanuni ya Petro.” Ambapo mtu husimamia tu pointi au wazo asilolijua. Lazima tuwe makini na hayo tukiwa tunahubiri. Kama hufundishi darasa la vijana kuhusu mawasiliano, kwanini ushindwe? Kama hufundishi na wala hujihusishi na kujifunza Biblia katika makundi madogo madogo, au kuwa mshauri katika vikundi vya kujisomea Biblia ukiwa na watu wanaokufanya wewe uwajibike, kwanini ushindwe? Kwanini umejiweka mwenyewe sehemu hizo ambazo unajifunza neno linasema nini, ambapo unajishusha chini kwenye neno hilo na unashindwa kuhubiri? Nitahimiza sisi wenyewe na watu wetu, tuanze kusoma kiundani Biblia katika makundi katika maisha yetu ama kanisani.

Mwishowe nahimiza kuwa na lengo madhubuti la kuhubiri kwa ufafanuzi katika kila mahubiri. Kwa uhakika naamini kwamba mahubiri mazuri ya ufafanuzi ni pale ambapo unawafanya watu/unawaalika kufikiria na wewe kwa muda mrefu, kupitia maandiko, kitabu, kupitia Biblia nzima. Wahimize/wafanye watu wako wafanye mazungumzo na wewe.

Nina neno, kutoka katika Waraka wa Pili wa Paulo kwa Wathesalanike. Kitabu cha kwanza cha agano jipya ambacho Paulo alikiandika ni barua alizoziandika na kutoka Athens kwenda kanisa la Thesalonike kwa kipindi hicho yalikuwa makao makuu ya Macedonia. Aliandika barua mbili kwa kanisa hilo kwasababu kulikuwa na mambo/pointi kadhaa zilizokuwa zikiwachanganya, lakini vile vile aliwathamini/heshimu kwa kuwaomba wao msaada. Neno hili hupatikana katika Sura ya tatu ya Wathesalonike wa I I . “ Mwishowe, kaka na dada zangu, ombeni kwaajili yetu, ili neno la Bwana lishike kasi na lilete faraja kama lilivyofanya kwenu ninyi.” Naupenda mstari huu: Maajabu ya yote ni kwamba Roho Mtakatifu atatutumia sisi, na lazima tuombe kwa hilo kuliko yote.


Reprinted by permission of Fuller Theological Seminary